

KUNG'ANG'ANIA



Asante, Ndugu, asante. Asante, Ndugu Joseph.

Na tuinamishe vichwa vyetu, kwa muda kidogo tu, kwa . . .

² Baba yetu wa Mbinguni, tuna furaha, leo, kuwa hai na kuwa hapa, tukiwa na nafasi, mara nyingine tena, kuhubiri Injili, utajiri wa Yesu Kristo usiotafutika. Nasi tunaomba ya kwamba, tunapomleta kwa watu, leo, katika umbo la Neno lililoandikwa, jalia Roho Mtakatifu alihuishe Neno kwetu sote, tupate kujiandaa kwa ajili ya Kuja Kwake. Tunaomba hayo, katika Jina Lake. Amina.

³ Mwaweza kuketi. Kuna jambo fulani tu maalum kuhusu Chicago, na kila wakati ninapokuja Chicago linaonekana zuri tu kwangu. Tangu mara ya kwanza kabisa nilipopata kuwa hapa kuhudumu, mimi daima, inaonekana kana kwamba kuna kitu fulani maalum kinachonivutia Chicago. Nami ninakuja sana, hata nadhani mnachoka kuniangalia, lakini ninyi ni mji mkuu sana, na wengi sana hapa, yapata watu milioni tano, nadhani, ama kitu karibu na hicho, ambao labda ningetaka kuwatembelea wote kuona kama wote wako kama hawa wanaohudhuria huu mkutano, kama ndivyo walivyo, ni mahali pazuri sana pa kuwepo, kwa kuwa uwepo wenu daima huleta mazingira mazuri sana ya imani ya Kikristo na ushirika, daima ni majaliwa kuwa hapa.

⁴ Mara yetu ya kwanza kuja ilikuwa ni kwa mwaliko wa maskini Ndugu yetu Joseph Boze. Na sasa, kwa kuwa Wafanyabiashara Wakristo wana tawi hili zuri sana hapa, na—na, nimealikwa mara nyingi nao, pia na kundi hili zuri la wahudumu la watu wa full Gospel kote Chicago. Kwa hiyo ni, ninahesabu haya kuwa ni majaliwa makuu sana ku—kuwa hapa leo, na kumwona Ndugu Sonmore. Nasi tulikutana nao jana jioni baada ya i—ibada, na kuwauliza kama walikuwa wakishuka kuja, nao hawakuwa na hakika sana, lakini naona hapana shaka Roho Mtakatifu aliwaongoza hapa kwa vyovyote vile.

⁵ Tulishukuru. . . Jana usiku tulipokuwa tukizungumza, mimi na mwanangu tulikuwa tumeketi pamoja tukiwa, sikuwa nimekula jana, na kwa hiyo nilikuwa nikila sambusa ndogo jana usiku, tulikuwa tukizungumza jinsi Ndugu na Dada Sonmore walikuwa watu mashuhuri, na ni kwa nini tuliona kuwa ni majaliwa makubwa sana kuwa na ushirika na kuwajua. Naye huyu hapa huku chini Chicago pamoja nasi leo. Bwana awabariki.

⁶ Nadhani mpenzi wako alikuja pia. Ninajua unajisikia hivyo juu yake, yeye angali ni mpenzi wako. Na hivyo ndivyo sisi, ninajua sisi, sisi sote Wakristo tunajisikia hivyo kuhusu wake

zetu kwamba wao wangali ni wapenzi wetu. Natumaini kamwe halibadiliki katika familia yangu, wala kamwe halibadiliki katika familia yenu, kwamba sikuzote tunaweza kujisikia hivyo kuhusu wake zetu, hata hivyo, wanasimama bega kwa bega pamoja nasi kutusaidia kupigana vita hivi, nasi tunawahitaji. Ingawa nimewaambia mambo mengi machungu sana, bali haikuwa kwa njia ya kuwafanya wajisikie vibaya, ilikuwa ni njia ya kuwaweka sawa na Injili.

⁷ Na mnaona, hicho ni chombo cha Shetani, mahali anapofanya kazi kwa nguvu sana, hicho kilikuwa ndicho chombo chake cha kwanza, kamwe hajabadilika. Yeye hukaa papo hapo kuninii. . . naye ni. . . Inatubidi tu kuwaombea dada zetu sikuzote, bila shaka, wao wanatuombea, pia, na pamoja, tukiwa pamoja, tunasonga mbele kama jeshi lisiloshindwa, pamoja na Jemadari wetu Mkuu, Kristo Yesu, huku Neno Lake likitutangulia, likitutengenezea njia.

⁸ Sasa, na kuwa hapa pamoja na Ndugu Carlson, ambaye ni, nisingeweza kusema maneno jinsi ninavyomthamini Ndugu Carlson. Mara nyingi ambazo nimekuwa, ameniona mahali ambapo ningebwagwa chini na kusimama pamoja nami, na—naye angali a—anathibitika kwamba ni ndugu halisi. Ninamthamini Ndugu Carlson. Ninawathamini ninyi nyote, Bwana awabariki vyema.

⁹ Sasa, ninajua mtakuwa na ibada kanisani mwenu baada ya kitambo kidogo. Nami ninawathamini wachungaji wenu, ambao ni wazuri ku—kusema kwamba kutakuwa na ibada hapa, nami ninawaona wawili kati yao wameketi jukwaani, labda, nadhani, na halafu wengi wao huko nje mkutanoni, huku nje kwenye kusanyiko; tunashukuru sana.

¹⁰ Nawatakeni mkumbuke ya kwamba kesho usiku ni mkutano huu wa kimishenari, kama ninavyouta, kwa ajili ya Ndugu yetu Joseph, nasi tutakuwa papa hapa. Nadhani tayari wameutangaza, mahali pengi na kadhalika.

¹¹ Na asanteni kwa maombi yenu ya siku chache zilizopita, nilipofikia nusura nisiwe pamoja nanyi tena hapa duniani, wakati bunduki ilipolipukia mkononi mwangu, chini kwenye uwanja wa shabaha. Mtu fulani alikuwa amenipa bunduki ambayo haikuwa, ilikuwa ni bunduki iliyotobolewa upya, wala haikuwa ni aina ya risasi ambayo, kwa kweli, ilipaswa kutumiwa nayo, ila kiwanda kilisema ilikuwa salama kabisa, ambapo kama ingalikuwa imetobolewa vizuri, ingekuwa, lakini kulikuwa na nafasi ya mbele, iliyoifanya risasi ilipukie nyuma usoni mwangu badala ya kutokea kwenye mtutu. Ndipo yapata tani sita za presha zikanipiga moja kwa moja usoni, na, ambayo iliivunjavunja hiyo bunduki, na kuurusha huo mtutu kwenye safu ya yadi hamsini, nayo bolti ikaenda upande mmoja, nayo

bunduki ikayeyukia mkononi mwangu. Nami hapa nimesimama alasiri ya leo ningali hai, Mungu na ashukuriwe, um-hum.

¹² Walitaka kuyachunguza macho yangu kuona. . . Kulikuwa na marisau mengi sana usoni mwangu, ilionekana kana kwamba ungechukua kipande cha sambusa, konzi yake moja, na kuiweka tu usoni mwangu, na kuna sehemu moja tu ndogo, ama mbili, papo *hapo* kwenye kipaji, ambayo ungeweza kuona, iliyosalia. Katika siku chache tu, ilikuwa yote, yapata siku tatu yote ikatoweka.

¹³ Kuna daktari mtaalamu, walinipeleka upesi huko wapate kuangalia waone kama yoyote ya hayo yaliingia kwenye mboni ya jicho langu. Ndipo akatikisa kichwa chake, na kuandika tena, na kusema, “Jambo pekee nijualo, ni kwamba hapana shaka Bwana mwema wa Mbinguni alikuwa ameketi pale pamoja na mtumishi Wake, maana mtu aliyemwokota, aliyemwona hakupaswa kupata kitu ila tu sehemu ya chini ya mwili wake, kitu chochote ambacho kingelipua bunduki kwa presha hiyo,” inchi moja kutoka jichoni mwangu, “kingeling’oa kichwa pamoja na mabega.” Kwa hiyo, mnaona, Mungu angali ni mwema, na Yeye. . .

¹⁴ Shetani hujaribu kutuua, bali hawezi kutuchukua mpaka Yeye aseme, “Tayari.” Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Kamwe hawezi kutuchukua, na kwa hiyo tunashukuru kwa ajili ya jambo hilo.

¹⁵ Nami ninashuk-. . . kwa Mungu kwamba Yeye amenipa nafasi ya kuendelea kubaki hapa duniani kuwaletea watu Wake Ujumbe ule ule niliowaletea: “Neema ya ajabu! Jinsi inavyosikika tamu!” Siku moja wanatarajia kutumia Umilele pamoja nawe.

¹⁶ Na wengi wa makundi hayo waliposikia habari zake, hatukusema lolote, kwa namna fulani tulinyamaza tu, bali simu ikilia, watu wakipiga simu, makundi ya maombi yamekusanyika kila mahali, yakifanya makundi, na kusema, “Vema, hatujui kama atatusikia ama hatatusikia, bali hakika tunaomba.” Hao ndio aina anaowasikia, hiyo ni kweli, hayo makundi madogo manyenyekevu, nami ninawashukuru.

¹⁷ Na jana jioni, kabla hatujaondoka kwenye uwanja wa mkutano, Ndugu Carlson alilifanya kundi lote kusimama, kasema, na kuniombea hilo, ili Mungu anisaidie. Na hilo linanifaidi sana, kwa sababu ninategemea maombi hayo.

¹⁸ Nami nikijua, hata hivyo, ya kwamba siku moja, Yesu akikawia, ni—nitaninii, itanibidi kuondoka. Halafu ninataka, “kuachana huacha nyuma yangu kumbukumbu za kudumu,” kwa Injili, Injili, nguvu za Mungu kwa Neno Lake. Ninataka kupanda Mbegu, ili kwamba wakati M—Mvua itakaponyesha, Roho Mtakatifu, Hiyo itachipusha, ipate Uzima, aina ya Mbegu ambayo nimepanda: Mbegu ya Biblia itakayoleta Kanisa la

Biblia, ambayo itamzaa Mkristo anayeamini Biblia ambaye ataamini, kumleta Roho Mtakatifu wa Biblia katika matendo, kwa sababu Neno liliandikwa na Roho Mtakatifu.

¹⁹ Naye ajapo, Yeye hulichukua Neno Lake Mwenyewe, nami ninapenda tu kudumu na Hilo. Yeye anaweza kufanya mambo ambayo hayajaandikwa *Hapa*, lakini ninatumaini tu kwamba ninaweza kuishi muda mrefu kutosha kumwona Yeye akitenda yote aliyoahidi *Hapa* ndani, hilo litakuwa tu sawa kwangu.

²⁰ Sasa, ni vizuri sana kuwa hapa, na kutazamia kesho usiku. Ningetaka kuitisha usikivu wenu kwa fungu dogo tu hapa ningependa kutumia kwa yapata dakika thelathini au arobaini, Bwana akipenda.

²¹ Naye Ndugu alikuwa amesema kwamba, loo, alitangaza kuwaombea wagonjwa, nami nilikuwa nimesahau kuwaambia wasambaze kadi za maombi, na, ila Mungu hakika atatutengenezea njia, kwa njia fulani. Tutapanga mstari vizuri ama *kitu kama hicho*, mpaka tutakapowaombea wote. Vema. Kwa hiyo sisi, samahani, lakini kamwe ha—hatukuwazia.

²² Sasa, hebu tugeukie Injili ya Marko Mtakatifu, tafadhalini. Nina Maandiko machache hapa yaliyoandikwa, na kama ungetaka, una poseli yako, ungetaka kuyaandika ninapoyarejea alasiri ya leo, tungefurahi sana. Marko Mtakatifu, tunataka kuanzia na kifungu cha 7, ama, mlango wa 7, na kuanzia kifungu cha 24, Marko Mtakatifu 7:24.

²³ Jicho langu la kulia, ambapo vile vipande kumi na vitano vya marisau viliingia chini tu ya jicho langu. . . Na marisau hayo yalikuwa na nguvu sana hata yakakwanyua magome ya miti, karibu yadi thelathini kutoka kwangu, nayo marisau madogo sana yakalipukia machoni mwangu. Ndipo daktari akasema, “Sijawahi kuona chochote. . .”

²⁴ Hayo marisau makubwa yamechomekwa kwenye fuvu la kichwa changu na kuzunguka mfupa wa shavu namna *hiyo*, yakalizinguka jicho langu, kipande kimoja kilipitia *hapa*, na kukata ncha ya jino *hilo*. Ndipo vipande kumi na vitano vikaenda chini tu ya mboni na kufanya duara ya nusu mwezi chini ya mboni, kamwe havikugusa mboni, vikarudi moja kwa moja jichoni, vikaingia ndani. Kipande kimoja kingeliigusa, jicho *hili* lingeenda. Na ndivyo ilivyo, kuvutwa kwa jicho kunalifanya tu dhaifu kidogo, bali litakuwa sawa, litakuwa sawa kabisa baada ya kitambo kidogo, ninamsifu Bwana kwa ajili yake.

²⁵ Hata tabibu mwenyewe alisema, “Sielewi, lakini,” kasema, “wakati hilo linapopata. . .” Mnaona, hilo lilitukia tu zaidi kidogo ya majuma mawili yaliyopita, kwa hiyo lingali ni dhaifu kidogo, bali alisema litakuwa sawa, nami nina hakika hicho ni kibali cha Bwana, litakuwa sawa.

26 Sasa, hebu tuanzie kwenye ninii ya the...aya ya 24 ya mlango wa 7:

Akaondoka huko, akaenda zake hata mipaka ya Tiro...Sidoni, akaingia katika nyumba,...lakini hakuweza kusitirika.

Kwa maana mwanamke mmoja, ambaye binti yake yuna pepo mchafu, alisikia habari zake, akaja akamwangukia miguuni pake:

Na yule mwanamke ni Myunani, kabila lake ni Msirofoinike; naye akamsihi aje amtote pepo katika binti yake.

Lakini Yesu akamwambia, Waache watoto washibe kwanza: maana si vizuri kukitwaa chakula cha watoto, na kuwatupia mbwa.

Naye akajibu, akamwambia, Naam, Bwana: lakini hata mbwa walio chini ya meza hula...makombo ya watoto.

Akamwambia, Kwa sababu ya neno hilo, enenda zako; pepo amemtoka binti yako.

Basi alipofika nyumbani kwake, akamkuta yule pepo amekwisha kumtoka, naye binti yake amelazwa kitandani.

27 Kama ningetaka kulipa anwani hili kwa ajili ya somo, ningeliita: *Kung'ang'ania*. Bwana na aongeze baraka Zake kwenye kusomwa kwa Neno Lake.

28 *Kung'ang'ania*, kulingana na kamusi ya Webster, nilikuwa—nilikuwa nikiangalia hivi punde, linamaanisha “kushikilia, kuninii...katika kutimiza lengo.” Huna budi kushawishika kabisa na kushikilia, ndipo unang'ang'ania. Na—nami, ni—ni neno zuri, ninalipenda, ni—ninalipenda sana neno hilo zuri, *kung'ang'ania*. Nami nafikiri huo ndio msimamo ambao Wakristo wote wanapaswa kuwa nao wakati wote, kung'ang'ania.

29 Nao watu katika nyakati zote, walio na imani katika yale wanayotaribu kufanikisha, daima wamekuwa wa kung'ang'ania. Kote katika historia ya wakati, watu ambao wamewahi kufanya lolote, wamekuwa watu wanaotaribu kufanikisha jambo fulani, nao hawana budi kuwa na imani katika yale wanayotaribu kufanikisha, nao wanapofanya hivyo, basi wanang'ang'ania.

30 Nilikuwa nikiwazia muda mfupi uliopita, nikiketi kwenye chumba cha moteli na kusema, “Bwana, niseme nini, alasiri ya leo, kwa watoto Wako? kwa kuwa nitashikilia kilichonunuliwa kwa Damu Yako kwa dakika arobaini na tano, ama saa moja, labda, alasiri ya leo, Wateule, watoto wa Mungu katika hili, ambao wanakaa hapa katika mji huu mkuu, na vitongoji vyake, wasafiri na wageni katika ulimwengu huu, hakuna mahali hapa

ambapo kweli wangeweza kupaita ‘nyumbani.’ Lakini Makao yao yako huko ng’ambo, nao ni wasafiri. Wala siwezi kuingia tu kwa urahisi kuwaambia watu hawa jambo fulani ambalo—ambalo huenda likawaudhi. Nami sina budi kusema jambo ambalo lingewasaidia.”

³¹ Siji kanisani nipate tu kuonekana ama kusikika, mimi—mimi huja kujaribu kuwasaidia watu hao, kujaribu kuwafanyia jambo fulani, wapate kuondoka kanisani, bila kusema, “Vema, niliketi pale, alasiri ya leo, bure, sikujiifunza chochote. Si—sikutembelewa na Roho.” Kwa hiyo, ninapenda kukaa katika Neno, kwa sababu Ro—Roho husafiri pamoja na Neno, na kusoma Neno Lake, na kuzungumza juu ya Neno Lake.

³² Ndipo nikaanza kuwazia juu ya *kung’ang’ania*, nami nikawaza, “Naam, watu wengi hung’ang’ania.” Kabla hujaweza kuwa mng’ang’anizi, huna budi kuwa na imani katika yale unayotaribu kufanikisha. Ina—inakubidi kwanza kuwa na imani kabla hujaweza kung’ang’ania, kwa hiyo imani na kung’ang’ania hutenda kazi pamoja, hao ni ndugu. Huna budi kuamini, la siyoy hutakuwa na, huna matumaini, hu—hu—hutajua kama uko sahihi au umekosea, lakini wakati umefikia mahali hapo ambapo una imani katika yale unayotaribu kufanya, basi unaweza kung’ang’ania.

³³ Nilikuwa nikiwazia, mwanzoni mwa historia ya taifa letu, wakati askari wachache kwenye siku ya baridi kali, huku hali ikiwa mbaya upande wao, hao walikuwa ni askari wa Marekani (Ninaposoma historia ya taifa letu, inanifanya nilie moyoni mwangu.), lakini kiongozi wao alikuwa Mkristo, Delaware ulikuwa umeganda, korongo za barafu ndani yake, nami ninasikia ya kwamba karibu nusu ya askari wa Marekani hata hawakuwa na viatu miguuni mwao, huku wamejizungushia vitu miguuni mwao, hao walikuwa ni askari wa Marekani, nazo pingamizi zilikuwa kubwa, mambo yalikuwa mabaya upande wao, lakini hata hivyo, baada ya maombi ya usiku kucha, mpaka akawa amelowa mpaka nyongani mwake kwenye theluji ambapo alikuwa amepiga magoti na kuomba, kiongozi wao mkuu akang’ang’ania, kwa kuwa alikuwa na hakikisho kutoka kwa Mungu ya kwamba angeweza kuvuka Delaware kwa vyovyote vile.

³⁴ Aling’ang’ania, ingawa matundu matatu ya risasi yalitobolewa kwenye nguo zake, alikuwa amesikia kutoka kwa Mungu, na haidhuru jinsi hali ya mambo ilivyokuwa, yeye angali, angeweza kung’ang’ania kwa sababu alisikia kutoka kwa Mungu na kuamini ya kwamba Mungu aliyekuwa akimwongoza kwenye ushindi kwa ajili ya taifa hili kuu alikuwa pamoja naye, hivyo basi kuganda kwa Delaware hakukumaanisha kitu kwake. Haidhuru kulikuwa na barafu kiasi gani, ama pi—pingamizi zilikuwaje, bado angeweza kung’ang’ania, kwa sababu alijisikia Mungu alikuwa upande wake.

35 Jinsi hilo lilivyo kuu, wakati tunapoweza kusikia kutoka kwa Mungu na kuwa, kuwa na hakika ya kwamba tuko moja kwa moja katika ushirika Wake! Basi hakuna kitu kikubwa kupita kiasi, hakuna kitu kikubwa vya kutosha kinachoweza kumzuia mtu huyo. Watu ambao wamewahi kuwa kitu chochote, wakati wowote, kupitia wakati wowote, wamekuwa watu waliomwamini Mungu na walikuwa na imani katika Mungu, na kusimama dhidi ya adui kila upande, nao waling'ang'ania kwa sababu walimwamini Mungu. Ninaamini kila Mkristo, kwa hiyo, anapaswa kung'ang'ania sana.

36 Ninawazia huko nyuma hapo mwanzo, kama tunavyoweza kuwazia juu ya yule nabii Nuhu mashuhuri. Alitoka katika familia ya Sethi, yenye haki, ambayo ilikuwa katika unyenyekevu. Kama ukipata kufuatilia nasaba za koo hizi, tunaona ya kwamba—ya kwamba watoto wa Hamu, ama, si Hamu, ninamaanisha watoto wa Kaini, wote walikuwa werevu, wenye elimu, wanasayansi, wafanyabiashara mashuhuri wa ulimwengu, lakini watoto wa Sethi walikuwa wanyenyekevu, watumishi wa duniani, walikuwa wachunga kondoo, nao walikuwa wakulima, na watu wanyenyekevu kwa tabia.

37 Basi hebu tuwazie juu ya Nuhu, mkulima wa kawaida tu huko makondeni akiwa na zana zake za kale, akijaribu kupata riziki kwa ajili ya watoto wake. Wala kamwe hakuwa msanifu hata kidogo, mtu mzuri tu, baraka za Mungu juu yake. Kila siku alipoingia nyumbani, angeikusanya familia yake anapokuja kula chakula chake cha aduhuri, na labda wote wangepiga magoti na kumwomba Mungu.

38 Siku moja alipokuwa huko nje kondeni, labda amefadhaika kabisa, nayo nafsi yake imehuzunika kwa sababu dhambi ilikuwa nyingi juu ya nchi, kwa sababu dhambi za hao watu zilikuwa zimepanda juu mbele za Mungu hivi kwamba ilimhuzunisha kwamba Yeye alipata kumwumba mwanadamu.

39 Kwa hiyo hapana shaka ilikuwa ni kitu kama wakati wa kisasa: majengo makubwa, marefu, mambo makuu. Mnajua, walifanya mambo huko nyuma katika sayansi ambayo hatuwezi kufanya siku hizi, walijenga piramidi na sfinksi, na mambo mengi waliyofanya ambayo hatungeweza kuyafanya siku hizi. Walikuwa na rangi siku hiyo, wangeweza kutia rangi katika kitu chochote ambacho kimedumu, hata wa leo, baada ya maelfu ya miaka; hatuna. Walikuwa na ustadi wa kuhifadhi maiti ambao hatuna siku hizi. Mambo mengi walikuwa wamefanikisha zaidi kuliko sisi leo hii. Ni ulimwengu mwerevu jinsi gani! Na basi lazima makanisa yao yalikuwa ni makubwa kuliko makanisa yetu siku hizi.

40 Lakini katika hayo yote, wakawa lundo la upotovu, kwa sababu ulimwengu ulikuwa umefunikwa kabisa na watu, wakiongezeka juu ya nchi, na ndipo vurugu ikaanza. Ninyi watu

hapa Chicago mna wakati mgumu zaidi kuiishia imani yenu ya Kikristo, kuliko mtu angekuwa nao huko mbugani, mahali fulani katika nyanda za magharibi, ambako haoni mambo, na upotovu, na vurugu ambazo iwakubidi kushuhudia kila siku, kwa hiyo inahitaji neema kuu na nguvu kuwaepusha na mambo ya ulimwengu.

⁴¹ Ana kanisa moja dogo lililoko huko nje mahali fulani, yeye na familia yake huendesha gari maili nyingi kwenda, Jumapili asubuhi. Labda haoni mtu mwingine yeyote mpaka yule mhubiri wa mzunguko atakapopita, ambapo watakutana tena. Hapa, kila siku mnakutana na mzozo kila upande, huku ibilisi akijaribu kuwashawishi *hivi* na *vile*. Ni vita kila saa ya maisha yako. [Ndugu fulani anasema, “Naam, ni vizuri, hata hivyo. Haleluya!”—Mh.] (Maana tuna ushindi mkuu, amina, Mshindi mkuu.)

⁴² Sasa, Nuhu, siku moja, alipokuwa huko nje nyandani, labda akilima, akitayarisha mazao yake, Mungu alishuka akaanza kuzungumza naye, kisha akamwambia Nuhu, labda kitu kama hiki: “Ninaweza kuona moyo wako, nami ninajua dhambi za ulimwengu huu zinakusumbua, kwa hiyo... Wote ni watu mashuhuri waliostaarabika, nao wameniacha kabisa. Nao ni watu wewevu, wenye elimu ya juu, watu walioadibishwa, lakini ninakutaka, kwa ajili ya kuokoa nyumba yako na wote watakaoingia, uende huko na kuanza kuandaa mashua kubwa, kwa sababu nitaleta mvua na kuuangamiza ulimwengu mzima.”

⁴³ Sasa, hapakuwa kumewahi kuwapo na mvua yoyote hapo kabla, na kwa hiyo sayansi ingemwambia, “Kwani mvua inatoka wapi?” na kadhalika. Lakini baada ya Nuhu kuishika Sauti ya Mungu na kuona mpango wa Mungu... Kuna jambo kuu ambalo wengi hukosa kuliona, ni mpango wa Mungu. Sasa, hakuna kitu kinachoenda kombo, ni sawa kabisa, kwa wakati kabisa, Yeye kamwe hachelewi, Kuja kwa Bwana kutakuwa kukamilifu kabisa, Kanisa litakuwa katika utaratibu kabisa wakati atakapokuja. Ninapenda hilo.

⁴⁴ Siku moja... Katika Mathayo 11:6 tunasoma mahubiri mafupi, Huenda nimelithubiri hapa wakati mmoja, juu ya *Heri Iliyosahauliwa*, wakati Yohana Mbatizaji, akiwa gerezani, aliagizia kuona kama Yesu kweli alikuwa Ndiye. Naye Yohana alikuwa ni mtu mashuhuri, naye alimpa Yesu sifa mbaya sana, lakini Yesu aliwambia, “Kaeni tu,” maana Yohana alikuwa na wasiwasi, huduma yake ilikuwa ikisema, “Anakuja Mtu ambaye pepeto Lake liko mkononi Mwake, Yeye atausafisha sana uwanda Wake, ataipeleka ngano ghalani, Naye atayateketeza makapi kwa Moto usiozimika.” Loo, jamani, ni Masihi wa jinsi gani ajaye!

⁴⁵ Lakini alipojitokeza jukwaani, ilikuwa ni tofauti, maskini Mtu mnyenyekevu, asiye na ushirikiano na madhehebu yoyote

kule. Nao...Hilo dhehebu lilikuwa tofauti, nao...Mahubiri Yake yalikuwa tofauti, Naye alisukumwa huku na huko, na kukimbia *huku* na kukimbia *kule*, kwa hiyo hilo lilionekana kidogo ni la kigeni, wasingeweza kulielewa. “Kwa nini? Kwa nini? Hakika nililhubiri, nao wanapaswa wote, wote kuliadini. Na hapa, ajapo, jamani, inaonekana kana kwamba nimeaibishwa.”

⁴⁶ Yesu hakuwaambia, “Sasa, nitawapa kitabu cha jinsi ya kujiadibisha gerezani, ninawatakeni, mumpe Yohana.” Alisema, “Kaeni tu mpaka ibada itakapokwisha, ngojeni tu mpaka ibada ya alasiri iishe.” Na wakati viwete walipotembea, vipofu wakaona, miujiza mikuu ikatendeka, Yeye alisema, “Enendeni mkamwonyeshe Yohana mambo haya, mwambieni niko kwenye wakati unaofaa, hakuna kitu kibaya. Niko moja kwa moja, kwa wakati, kabisa.”

⁴⁷ Na hivyo ndivyo Mungu alivyo siku hizi, Yeye yuko kwenye wakati kabisa. Wasiwasi wetu wote na kuhangaika kwetu hakutafaa kitu, ng'ang'ania tu kwa Neno la Mungu na uendelee mbele, Mungu yuko kwenye wakati mzuri kabisa, kikamilifu, kabisa. Kama vile vitu vyote, jua, mwezi, na kila kitu ambacho ni cha Mungu, hakina budi kufanya kazi kwa wakati.

⁴⁸ Sasa, Nuhu, baada ya kusikia jambo hili, ingawa hakuwa msomi, ingawa labda alichekwa, kama Biblia ilivyosema, walikuwa wenye kudhihaki, walimdhihaki, alijua yote yaliyokuwa mbele yake katika huo ulimwengu mkuu wa kisayansi, alikuwa na hakika kwamba ni vigumu kwa mtu yeyote kumwamini, lakini kwa miaka mia moja na ishirini alikuwa aking'ang'ania.

⁴⁹ Wakati alipojenga hiyo safina, akaweka mbao ndani yake na kuimiminia lami na kuitengeneza, watu walimcheka na kumdhihaki, bali alisimama papo hapo mlangoni na kuhubiri hukumu za Mungu zijazo, halikumzuia hata kidogo. Kwa nini? Alikuwa na imani katika yale aliyokuwa amesikia, “Kwa maana imani chanzo chake ni kusikia, kusikia Neno la Mungu.”

⁵⁰ Kwa hiyo haidhuru ni nini kinachoendelea, maadamu unadumu na Neno la Mungu, ng'ang'ania, haidhuru una ugonjwa gani, na yale daktari aliyosema. Huyu mtu mwema, labda akifanya yote ajuayo, bali yeye yuko katika ulimwengu wa kisayansi, sisi tuko katika ulimwengu wa kiroho, ambapo tumefufuka pamoja na Kristo, Uzima mpya, tumepita kutoka mautini kuingia Uzimani, sisi ni kiumbe kipya katika Kristo.

⁵¹ Kwa hiyo Nuhu aling'ang'ania sana na Ujumbe wake, hakuwa na woga. Haidhuru yeyote wao alisema nini, huenda walimwita chochote, hilo halikuukomesha hata kidogo, alikuwa na imani katika Neno la Mungu aliloambiwa, aliendelea moja kwa moja kujenga safina. Haidhuru wangeweza kuthibitisha kisayansi jinsi gani kwamba Ujumbe wake ulikuwa wa uongo,

kinyume, Mungu anaweza kuleta mvua angani, kama Neno Lake lilisema hivyo.

⁵² Mungu angeweza kumponya mwanaume anayekufa kwa kansa, wakati daktari amemkatia tamaa, ama mwanamke? Angeweza kumfanya kiwete atembe, na kadhalika? Anaweza kufanya hivyo, wakati hakuna kitu katika milki ya matibabu kinachoweza kuugusa? Huo—huo—huo ni ulimwengu *huo*. Huo ni ule ulimwengu mwingine, kama ilivyokuwa katika wakati wa Nuhu. Waliudhihakia ulimwengu alimoishi Nuhu, bali Nuhu akaendelea moja kwa moja na Ujumbe wake. Haidhuru wangeweza kuthibitisha *kisayansi* kiasi gani hayakuwako, kwa Nuhu yalikuwepo, kwa sababu Mungu alisema hivyo.

⁵³ Hivyo ndivyo ilivyo kwa mwaminio wa kweli siku hizi, haidhuru wanasema kiasi gani, “Huyo si Roho Mtakatifu, ni saikolojia. Ni namna fulani ya udanganyifu, ni telepathia,” chochote kile, hilo haliwazui watu wa Mungu hata kidogo. Wanajua Mungu alitoa ahadi ya kwamba siku hii ingekuwa hapa, kwa hiyo wanavumilia na kusonga mbele na Ujumbe. Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.” Mnaona?

⁵⁴ Kung’ang’ania, angeweza, kwa sababu alijua yale alikuwa anaenda kufanikisha. Naye alijua yale Mungu alikuwa ameahidi, naye alijua ya kwamba Mungu aliyaweka mkononi mwake. Wala haikumbidi kuchukua “la” au “ndiyo,” ama chochote mtu mwingine yeyote alichosema, yeye hakuwa akiangalia yale waliyosema, alikuwa akiangalia yale Mungu aliyosema. Na kwa hiyo, haidhuru hao wengine walisema nini, labda wenye dini wa siku hizo hakika hawakukubaliana naye, hakika walimpinga, kwa sababu hakuna mmoja wao aliyeokolewa, kila mmoja wao aliangamia, bali Nuhu alikuwa na Neno la Bwana, nayo, haikuleta tofauti yoyote kile walichosema, yeye aling’ang’ania.

⁵⁵ Huenda walimwita, “mwendawazimu, mtakatifu anayejibingirisha,” na baadhi ya majina hayo wanayowabandika waaminio siku hizi, hilo halikumkomesha hata kidogo, kwa sababu ha—hakuyasikiliza hayo, alikuwa na moja la kufanikisha: kujenga hiyo safina. Mtu yeyote aliyetaka kuingia, walikaribishwa kuingia, bali ilikuwa ni kazi ya Mungu kuwaingiza, yeye alihubiri tu Neno. Hivyo tu ndivyo tunavyopaswa kufanya leo hii, kudumu na Neno na kung’ang’ania.

⁵⁶ Musa, mtu mwingine aliyeng’ang’ania, alikuwa na mafunzo yote ambayo angeweza kupata huko Misri, alikuwa mwanajeshi, mtu mashuhuri. Naye, katika nguvu zake za kijeshi, ama, kwa nguvu zake za maarifa yake mwenyewe, alitoka kwenda kuwakomboa Israeli, kwa sababu alijua wakati wake wa kutukia ulikuwa umewadia. Lakini aliwazia, moyoni mwake, ya

kwamba watu walikuwa wamefunzwa vya kutosha kuelewa ya kwamba ule wakati ulikuwa umewadia, naye alikuwa ndiye mtu aliyekuwa amekuja kuwasaidia, lakini hawakuelewa. Kwa hiyo unaona hayo magurudumu hayakugongana pamoja, kulikuwa na kasoro.

⁵⁷ Na wakati Mungu anapoweza kuzungumza katika mkutano, na kama magurudumu hayako pamoja, haitakufaa chochote. Huna budi kujiweka sawa na ahadi Yake, huna budi kupanga njia yako ya kuwazia, si yale mtu mwingine aliyosema, ama mtu fulani *hapa* aliyosema, ama madhehebu fulani yaliyosema, ama—ama daktari fulani aliyosema, huna budi kujiweka sawa na ahadi ya Mungu, ndipo uisikie Sauti Yake ikinena na kusema, “Ni *wewe*.” Ndipo unang’ang’ania, ndugu, hakuna kitu kitakacholizuia basi. Ni kweli. Lolote linaweza kutukia, bali kamwe halitakuchukua, unaweza kung’ang’ania, kwa sababu hatuwezi kufa, tayari tumekufa. Tuna arabuni ya wokovu wetu, sasa hivi, kwa sababu tumefufuka pamoja Naye, tumefufuka pamoja Naye, na tumeketi katika ulimwengu wa Roho, sasa hivi, tukiwa na hakikisho.

⁵⁸ Nilikuwa nikizungumza hivi majuzi usiku na kusema, “Kama vile Israeli. . .” Sasa, hawakujua walikokuwa wakienda, walikuwa tu na nchi ya ahadi. Lakini kabla hawajafika kwenye nchi hii ya ahadi shujaa mkuu, jina lake Yohua, ambalo linamaanisha “Yehova, Mwokozi,” aliingia kwenye nchi ya ahadi na kuleta ushahidi kwamba nchi hiyo ilikuwako, jinsi tu Mungu alivyoahidi. Walikuwa na huo ushahidi, ndipo angeweza basi kung’ang’ania. Hiyo ndiyo sababu aliwatuliza Israeli katika hoja yao, wao walisema, “Hatuwezi kuiteka. Loo, ha—hatuna budi kurudi. Hatuna budi kufanya *hivi*.”

⁵⁹ Akasema, “Tunaweza hata na zaidi kuiteka!” Kwa nini? Alikuwa akiangalia yale aliyosema Mungu, naye alikuwa na ushahidi.

⁶⁰ Wakati Yesu alipojitokeza jukwaani, Yeye alituhidi Nchi, “Nyumbani mwa Baba Yangu mna makao mengi. Na kuna Uzima ng’ambo ya mauti.” Naye akavuka Yordani, kile tunachoita “Yordani,” mauti, alivuka akaingia kwenye ile Nchi nyingine na kuleta ushahidi, kwenye siku ya tatu akafufuka tena; alikula, akanywa, kisha akasema, “Niguseni Mimi, Mimi si roho, Mimi ni nyama na mifupa.” Kisha akasema, “Nitawapa Arabuni ya jambo hili, lakini ngojeni huko juu siku kumi.” Wakang’ang’ania baada ya hilo pia, kwa sababu walikuwa na zi—zile nguvu, Ushuhuda wa ufufuo ndani yao. Hiyo ndiyo sababu hawakupenda maisha yao hata kufa, kwa sababu wanguweza kuvumilia, walikuwa na Ushahidi, wa—walikuwa wamefanikisha jambo fulani kupitia kifo cha Yesu Kristo.

⁶¹ Je, Yeye anamaanisha hivyo kwako alasiri ya leo? Je, unaweza kung’ang’ania katika kusema, “Ninaamini. Hata iweje,

ingali ni yangu, kwa sababu tayari nimefufuka pamoja Naye katika ufufuo. Ninaangalia nyuma, na kuona maisha niliyoishi wakati mmoja siyaishi tena.” Kuna shida gani? Hiyo inaonyesha ulikufa pamoja Naye na umefufuka pamoja Naye, nawe una Arabuni, Malipo ya kwanza, juu ya ufufuo wako wa Milele.

⁶² Naam, Musa alishindwa. Lakini siku moja...Mwajua, Musa hakuwa amewahi kuisikia Sauti ya Mungu, alikuwa tu ameambiwa na mama yake na walimu wa siku hiyo, *hiki-nahiki* kilikuwa kinakuja, Mungu atatuma mkombozi. Mama yake akasema, “Mwanangu, ninaamini wewe ndiwe mtu huyo.” Musa hakujua kwa hakika, asingeweza kuelewa, kwa hiyo kosa dogo la kwanza lilipotokea, kasoro ndogo ya kwanza, tishio dogo, akakimbilia nyikani.

⁶³ Lakini siku moja, alipokuwa akichunga kondoo, aliona kichaka kilichowaka moto, na kutoka kwenye hicho kichaka kilichowaka moto ikaja Sauti, nayo ikasema, “Hakika, nitakuwa pamoja nawe.” Aling’ang’ania. Kwa nini? Alikuwa na imani. “Nitakuwa pamoja nawe.”

“Mimi—mimi ni mtu wa ulimi mzito.”

Akasema, “Ni nani anayemfanya mtu kiziwi, ama bubu, au kunena?”

“Uh, hawataniamini.”

“Nitakuwa pamoja nawe.” Ndipo akang’ang’ania.

⁶⁴ Alipoingia mle mbele ya Farao naye akaona baadhi ya watu hao wakijaribu kuninii. . .

⁶⁵ Ninafanya jambo baya hapa, nadhani? Mimi. . .Ninatembea kupita kiasi. Hilo ni sawa. Asanteni. Samahani, Ndugu. Nadhani ninakuziba maskio pia, kama ungefuatilia hilo kidogo, mimi. . . ingekuwa bora zaidi, labda. Mimi. . .

⁶⁶ Huko chini katika—katika Misri, Musa aliingia katika mapambano. Na kwa hiyo, mtu hana budi kujua anachozungumzia kama utang’ang’ania. Kwa hiyo, akaingia katika mapambano, akakutana na baadhi ya waigaji waliokuwa wakijaribu kufanya jambo lile lile alilofanya, nao wakafanya hivyo, kwa kiasi fulani, bali hilo halikumkomesha, aling’ang’ania. Kwa sababu...Aliwaona wenye kudhihaki jambo lililo sahihi, akaendelea tu mbele moja kwa moja, kwa sababu alijua ya kwamba Mungu alimtuma. Na kwamba matokeo yake ni nini, hiyo ni juu ya Mungu.

⁶⁷ Wakati Israeli walipolia, yeye alishikilia, “Tunasonga mbele.” Walipotaka kurudi, alisema, “Tunasonga mbele.” Aling’ang’ania, naam. Alishikilia. Kung’ang’ania, jamani, hilo linamaanisha nini kwetu leo! Watu wa nyakati zote, wanaomwamini Mungu, hung’ang’ania.

⁶⁸ Mwangalie Daudi. Maskini Daudi, bila shaka alilelewa katika nyumba nzuri, ya kuamini, baba yake, Yese, mtu

mashuhuri wa Mungu, bila shaka aliwakusanya wavulana hao wote usiku na kufanya maombi ya familia kabla hawajaenda kulala, labda alisoma yale magombo, na akazungumza juu ya Yehova mkuu Ambaye alikuwa amefungua Bahari ya Shamu, naye nabii mkuu Musa alikuwa amewatoa, akiifuata Nguzo ya Moto, mambo haya yote, hiyo iliumba imani, “Imani chanzo chake ni kusikia, kusikia Neno la Mungu.” Maskini Daudi akaanza kuwazia jambo hilo.

⁶⁹ Loo, bila shaka, yeye alikuwa, kwa namna fulani ndiye mdogo kuliko wote wa familia, kwa hiyo wakamtoa nje akawachunge kondoo wachache, naye aliwajibika kwa hao kondoo. Ndipo siku moja simba akaja na kumchukua mmoja, naye akawaza, “Sasa, nitamwambia nini baba yangu kuhusu kondoo huyu kupotea?” Ndipo ikawa alikumbuka kwamba “Baba yangu alisoma kutoka yale Magombo na kuniambia ya kwamba Mungu alikuwa ni Mungu mkuu kuwakomboa watu Wake, na kwamba angewabariki Israeli, na alikuwa pamoja na Israeli. Nami ni mmoja wao, na wote waliotahiriwa, na katika agano hilo, baraka za Mungu ziko juu yao, nami ni mmoja wao. Nimetahiriwa, na baraka za Mungu ziko juu yangu, nina haki. Mmoja wa kondoo wa baba yangu amepotea, kwa hiyo ninamfuatilia kondoo huyo.”

⁷⁰ Ndipo akanyakua kombeo lake dogo, akaenda, na kumrudisha huyo kondoo kwa kumwua huyo simba. Kwa nini? Aling'ang'ania. Mungu alikuwa akifanya nini? Kumfundisha. Dubu aliingia na kumkamata mmoja, akaenda akamtoa huyo kondoo kwa huyo dubu.

⁷¹ Siku moja, alipowapelekea ndugu zake chakula, wakati majeshi yalipokuwa moja ng'ambo ya handaki kutoka kwa lingine, bonde dogo ambapo kijito kidogo kilipitia kati yao, basi kulikuwako na Goliathi mkubwa huko nje, akikigamba. Labda Daudi alimtizama, akarudi, akaangalia huku na huku kidogo, kuona ni nani. . . akaangalia juu, aone ni nani aliye mkubwa kuliko wote, na mtu—mtu mkubwa kuliko wote jeshini, basi ilikuwa ni Sauli, yule kiongozi, mrefu kuliko wote tangu begani hadi kichwani.

⁷² “Vema, kwa nini asiende huko nje?” aliwaza. Akaendelea mbele, nadhani alikuwa akiwazia, “Mungu, Baba yangu, najua kama Wewe unajali kiasi *hicho* mmoja wa hao wana-kondoo huko nje, unawajali kiasi gani watu wanaoitwa kwa Jina Lako? Sasa, wanapambana, na wote wanaogopa.” Naye akavumilia sana, akaanza moja kwa moja kumfuata Goliathi kwa kombeo lile lile na kupata ushindi. Kwa nini? Aliamini katika yale aliyokuwa akijaribu kufanikisha. Mafanikio yake yalikuwa sahihi, yalikuwa katika mapenzi ya Mungu, katika Neno la Mungu, katika mpango wa Mungu.

⁷³ Na kama unaweza kujua mahali pako ni gani katika mpango

wa Mungu, ingawa wewe ni mgonjwa na karibu umekufa... Unasema, “Mimi ni Mkristo, hilo lingewezaje kuwa katika mpango wa Mungu?” Huenda ikawa katika mpango wa Mungu kukuponya na kukupa ushuhuda ambao utawatikisa watu waingie kwenye Ufalme wa Mungu. Bila shaka. Yeye huacha mambo hayo yatendeke. Labda ulikuwa na pata potea zako na adui akikuunguza huku na huku, huenda ilikuwa hivyo. Hayo yote yako katika mpango wa Mungu.

⁷⁴ Mwangalie Ayubu, wakati alipoteseka, amejaa vidonda mwilini mwake, yote yalikuwa katika mpango wa Mungu, lakini Ayubu, pia, aling’ang’ania kwa sababu alijua ya kwamba alikuwa akilitimiza Neno la Mungu, hakuna kitu kingesumbua.

⁷⁵ Ningeweza kuwazia, leo, juu ya Samsoni, aling’ang’ania pia. Alikuwa aking’ang’ania maadamu angeweza kuona ya kwamba ile ahadi ya Mungu ilikuwa pamoja naye. Kila wakati ambapo Wa—Wafilisti wangejigamba, ama kumsukuma kwenye kona... Huenda ikawa maskini mikono midogo iliyokonda, na maskini jamaa mdogo dondoadume mwenye vishungi saba vidogo vya nywele vilivyoning’inia chini, ambaye wote walimwita, “Dondoadume,” na, lakini angepapasa-papasa karibu aone kama vishungi hivyo vilikuwa sawa, aliwaacha tu simba wangurume, akawaacha Wafilisti wamfungie, wafanye lolote walilotaka, angenyanyua malango yote ya mji na kuyabeba juu kilimani. Kwa nini? Aling’ang’ania. Kwa nini? Aliona, na kugusa, na kujua ya kwamba ahadi ya Mungu ilining’inia juu yake. Amina. Hmm!

⁷⁶ Ninyi Wapentekoste mnapaswa kufanya nini mnapomwona Roho Mtakatifu akitenda kazi miongoni mwetu? Mnamwona akifanya ishara na maajabu, akiwachukua wenye dhambi na kuwafanya watakatifu, akiwachukua wagonjwa na kuwaponya, akiwafanya vipofu kuona, viziwi kusikia, na hata kuwafufua wafu, akifanya ishara na maajabu ya kila namna, halafu tunaketi nyuma kama kundi la watoto wachanga walioshindwa. Kile tunachopaswa kufanya ni kung’ang’ania! Kusimama pale na kumwamini Mungu...

⁷⁷ Kuhisi Roho Wake akipitia juu ya nafsi zetu katika nguvu za kufufuka Kwake, kisha turudi kwenye Neno Lake, tuseme, “Waweza kuniombea tena?” Ati kuniombea tena? Mungu alitoa ahadi, kisha Yesu akafa mara moja, hilo latosha, hivyo tu. Basi ng’ang’anieni. Naam, bwana, iweni kama askari halisi. Loo, jinsi Yeye alivyo mkuu!

⁷⁸ Maadamu Samsoni alijua ya kwamba karama yake ilikuwa pamoja naye, angeweza kuhisi hivyo vishungi saba, angeweza kukabiliana na Mfilisti yeyote. Mbona, aliokota mfupa wa taya la nyumbu na kuwabwaga chini Wafilisti elfu moja! Ungeweza kuwazia jambo hilo? Sasa, hilo ni moja kwa ajili ya

wanasayansi siku hizi, sayansi. Maskini mfupa wa taya, hivi uliwahi kuona mfupa ukiisha kuwa, kukaa kwenye, umepauka namna hiyo? Mbona, umeoza uwezavyo kuwa, ugonge tu nao utaruka vipande-vipande. Na hizo helmeti zilikuwa na unene wa kama inchi moja na nusu, juu ya vichwa vyao pamoja na deraya kubwa juu yao, ambayo labda ni inchi nyingine.

⁷⁹ Jamaa wakubwa mno, mikuki mikubwa mkononi mwao, na hapa maskini mduvi huyu mwenye nywele za kipilipili alisimama pale nje akiwa na mfupa wa taya, na kuyaponda-ponda hayo mafuvu ya vichwa moja kwa moja, na kuwaua elfu moja akiwa peke yao. Mbona, hakuogopa! Kwa nini? Alihisi, aliona hivyo vishungi vilikuwa vingali vimening'inia pale, ndipo akang'ang'ania sana.

⁸⁰ Maadamu Mkristo anaweza kujua ya kwamba anaishi juu ya dhambi, kwamba Roho Mtakatifu anambariki na kusimama pamoja naye, atang'ang'ania na kukaza mwendo kuifikia mede ya wito mkuu. Wakristo wanapaswa kuwa hivyo, kung'ang'ania sana katika madai yao kwa Mungu, wadumu nayo.

⁸¹ Nilizungumza, dakika chache zilizopita, kuhusu Yohana Mbatizaji, ningetaka kusema jambo lingine kabla sijaliondokea hilo. Mwajua, Yohana kidogo alikuwa mtoto wa kipekee. Hatuna historia nyingi sana kuhusu maisha yake, tunajua baba yake alikuwa ni kuhani kutoka shule ya elimu, Zekaria, mama yake alikuwa Elisabeti, mke wa kawaida tu wa nyumbani, walikuwa wakongwe, ndipo Mungu akamtokea siku moja, kwa Malaika, Gabrieli, na kumpa a—ahadi ya huyo mtoto.

⁸² Na hapana shaka kwa namna fulani iliuhuzunisha moyo wa hao mume na mke wakongwe, kwa sababu walijua ya kwamba mvulana huyo atakuwa kiongozi wa Mungu, atakuwa mtu mashuhuri sana, walijua ya kwamba angepitia majaribu na dhiki za kila namna, na kupingwa na watu, na kila kitu, maana daima wako hivyo. Kama sivyo walivyo, huu wakati una kasoro. Hiyo ni kweli.

⁸³ Kwa hiyo basi, tunaona ya kwamba hapana shaka kwa namna fulani lilikuwa ni jambo la kuvunja moyo kwa hao mume na mke wakongwe, wakijua ya kwamba itawabidi kufa na kumwacha mvulana huyu, kabla hawajamwona huyu mwana wao akiingia katika upako wake mkamilifu apate kuwa m—mtangu- . . . kiongozi, ama, hasa, mtangulizi wa Masihi ajaye, waliamini hilo, na labda walimwambia hivyo.

⁸⁴ Sasa, Yohana alipokuwa angali katika ujana wake, baba yake na mama yake walikufa. Na ilikuwa ni ajabu, kijana huyu ambaye Mungu alikuwa amemwita, si ni ajabu sana kwamba hakufuata utaratibu wa dini ambayo baba yake alikuwa mfuasi wake? Kweli, ilikuwa ni desturi ya siku hizo kwamba watu . . . U—ukuhani ilibidi utoke kwa Lawi, bila shaka. Kwa hiyo

alikuwa . . . Walawi walikuwa makuhani, nao walienda kwenye hekalu lao na kujifunza taratibu zote.

⁸⁵ Lakini mnajua, Yohana hakufanya hivyo, tunaambiwa ya kwamba Yohana alitoka akaenda nyikani. Hakutaka kujichanganya katika mapokeo yao, alikuwa na kazi muhimu, naye mwanadamu alikuwa ameivuruga kabisa. Kwa hiyo yeye, kama alikuwa awe na hakika . . . Ilibidi awe ndiye wa kumtambulisha Masihi, naye ilimbidi kuwa na hakika ya kwamba Huyu alikuwa ni Nani.

⁸⁶ Kwa hiyo labda, kama angaliwaendea makasisi na kusema, “Mimi ni mwana wa Zakaria”: “Ingia ujiandikishe na—na ulipe karo yako. Waliuza ile nyumba kule juu, na—nasi tutakufunzia hapa, nawe utatumika mezani,” na kadhalika. Loo, jamani! Akaenda kwenye seminari yake na kujazwa kasumba kabisa, na kufundishwa kabisa, na kadhalika namna hiyo.

⁸⁷ Wangesema, “Sasa, kama utamtambulisha Masihi, vipi kuhusu kuhani wetu mkuu, leo hii? Hivi huoni yeye ni mtu mzuri? Angalia *jinsi* anavyoweza kusimama, na *jinsi* anavyoweza kuinama. Hivi huoni huyo anaonekana kama Masihi? Labda huyo Ndiye.”

⁸⁸ Loo, huyo kasisi mwingine angalisema, “Loo, la, la, la. Umekosea, isingekuwa ni mzee, kama huyo, ingekuwa ni huyu kijana mwanamume *hapa*, huyu mwinjilisti kijana anayeiwasha moto nchi. Unajua ya kwamba huyo angekuwa ni Yeye. Mbona, angalia, mbona, anaweza kunukuu kanuni zetu zote za imani na kadhalika, anajua mapokeo yote ya wazee kuliko mtu mwingine yeyote. Naye ni mtu mashuhuri sana! Kila- . . . hata Mafarisayo, Masadukayo, na Waherodia, wote wanashirikiana naye. Yeye ana huduma iliyo kuu kuliko zote uwanjani siku hizi. Huyu ndiye yule jamaa, Yohana.”

⁸⁹ Yohana hakutaka wajichanganye katika upuuzi kama huo, alikuwa na kazi muhimu. Alifanya nini? Alikaa pale mpaka aliposikia kutoka kwa Mungu. Mungu alisema, “Nitakwambia Yeye ni Nani. Wewe endelea tu huko nje, bali Yule utakayemwona Roho akishuka juu yake, Huyu Ndiye. Hiyo itakuwa ndiyo ishara ya Masihi. Wewe endelea mbele tu ukahubiri, na uhubiri toba, na kuwabatiza kwa toba, na kuwaambia ya kwamba Mimi naja. Lakini usiwaache wakulettee mtu fulani na kusema, ‘Mtawaze sasa na kumfanya askofu mkuu, ama kumfanya Masihi,’ ama chochote kile. Wewe ngojea mpaka utakapoiona ishara hii. Utakapoiona ishara hii, basi Huyu Ndiye, waambie Israeli, ‘Huyo Ndiye,’ unasema, ‘Huyo Ndiye,’ utakapoona ishara ninayokwambia uone.”

⁹⁰ Ee Mungu, tusaide leo! Sio, “Milioni moja zaidi katika mwaka wa ’44,” na upumbavu huu mwingine wote tulio nao, na damu, moto, moshi, na mvuke, na mambo ya kila namna, dumu

na Neno. Mihemuko ya kila namna, ibilisi anaweza kuiga kila mmoja wao. Dumuni na Neno.

⁹¹ Yohana alingojea, angewabatiza wachache kisha aangalie pande zote, angewabatiza wengine wachache, kasisi angesema, “Ni nani Huyu unayenena habari zake?”

⁹² Akasema, “Kuna Mtu anayesimama hapa mahali fulani.” Hivyo ndivyo alivyosema. “Kuna Mtu aliyesimama miongoni mwenu sasa, ninyi hamumjui, wala mimi simjui. Lakini Yeye Ndiye atakayebatiza kwa Roho Mtakatifu na Moto. Mimi ninabatiza tu kwa maji.”

⁹³ “Yeye ni nani? Aisee, nawaambia, ndugu yetu, ndio kwanza apate Ph.D. yake hivi majuzi, huyo Ndiye. Mvalisheni, mvalisheni joho lake, kofia yake ya kuhani mkuu,” ama chochote kile. “Mketisheni pale chini, hebu aonyeshe vitambulisho vyake, ana ushirika mzuri na kila mtu. Shuka uje huku. Huyu *ndiye*, Yohana?”

“Huyo si Yeye.” Amina.

⁹⁴ Kama vile mzee Samweli, nabii mwingine aliyemtangulia, kumpata mmoja kutoka kwa wana wa Daudi, uh, kutoka kwa wana wa Yese, samahani, akijaribu kumtafuta Daudi. Wakamleta maskini jamaa huyo mdogo, jamaa mwenye mabega yaliyoinama, aliyeonekana mwekundu, akasema, “Huyo ndiye, huyo ndiye.”

Kwa hiyo wakaninii, labda, labda waliwaleta wanatheolojia wao wote karibu, wakasema, “Je, huyu Ndiye? Huyu Ndiye?”

Yohana akasema, “La, hakuna hata mmoja wao, Mungu amewakataa wote. Sijui Yeye ni Nani. Lakini Yeye aliniambia kile ningeona.”

“Vema, angalia hapa, jamaa *huyu* ana shida gani?”

“Sijui. Lakini nina ishara fulani ambayo sina budi kuiona.”

⁹⁵ Ndipo siku moja, akashuka maskini Mtu asiye na sifa, ila tu jina jeusi, chafu nyuma Yake, aliyezaliwa mtoto haramu, ndivyo watu walivyodhania, naam. Akashuka akaenda pale pamoja na—na m—mtu jina lake Lazaro. Yohana akaangalia juu, aling’ang’ania kabisa, akasema, “Huyo hapo, Huyu Ndiye.”

“Unajuaje?”

⁹⁶ “Yeye aliyeniambia niende nikabatize kwa maji, alisema, ‘Yule ambaye utamwona Roho akimshukia na kukaa juu Yake, Huyu Ndiye atakayebatiza kwa Roho Mtakatifu na Moto.’” Aliitazamia ishara hiyo ya Masihi, aling’ang’ania.

“Unajuaje ni Yeye?”

“Ninajua ni Yeye.”

“Kwa nini? Sasa, hebu niambie. Tafuta hii... Na uende kwenye shule ya elimu. Unapata wapi hii?”

“Mungu aliniambia hivyo.” Aliisikia Sauti ya Mungu naye akajua ya kwamba alikuwa Ndiye.

⁹⁷ Maskini mwanamke huyu Myunani, itatubidi kuharakisha na kumfikia upesi sana, tuzungumze habari zake kwa dakika chache. Ninawazia alikuwa na matatizo fulani pia. Kwanza kabisa, tunaona ya kwamba alisikia habari Zake. Hilo ndilo jambo la kwanza kufanya, huna budi kusikia habari Zake. Alisikia habari Zake. Alisikia nini? Sifa Zake, kwamba Yeye alikuwa ni Nani. Hapana shaka mtu fulani mwema alikuwa ametangaza habari hiyo.

⁹⁸ Naye alikuwa na mtoto aliyekuwa mgonjwa, naye, hakuna kitu kingaliweza kumsaidia. Alikuwa anaogua, labda, kifafa, alikuwa na pepo ambaye, labda angemwua, angekuwa juu yake maishani mwake mwote. Alikuwa amesikia juu ya wengine kuponywa.

⁹⁹ Sasa, labda mtu fulani alikuwa amesema, “Sasa, ngoja kidogo, kwanza, huwezi kwenda kwenye kundi hilo, yeye ni Myahudi, yeye ni mfuasi wa dhehebu lingine. Huwezi, yeye anatoka kwenye kundi lingine, huwezi kumwendea.”

¹⁰⁰ Mnajua, kwa njia *fulani* imani hupata chanzo ambacho wengine hawajui chochote kukihusu. Haidhuru wanajaribu kiasi gani kusema, “Usiende,” wanaenda kwa vyovyote vile. Mnaona? Maana imani hupata chanzo chake, wengine hawakioni. Hiyo ni kweli. Sasa, yeye alijua Neno Lake. Nayo Biblia ilisema, katika Waebrania mlango wa 4 na kifungu cha 12, kwamba “Neno la Mungu ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, hukata hata ku—kuigawanya na—nafsi, na ni Mtambuzi wa mawazo ya moyo.” Hivyo ndivyo Neno la Mungu lifanyavyo, huyatambua hata mawazo yaliyo moyoni mwako.

¹⁰¹ Sikilizeni, imani ndio mkono unaoweza kuutumia Upanga huo. Hakuna mkono mwingine unaoweza kufanya hivyo, hakuna mkono wa kikanisa, hakuna mkono wa kimadhehebu, hakuna mikono ya kundi, hakuna mikono ya kitaifa, inahitaji mkono wa imani kufanya hivyo. Na inategemea jinsi mkono huo ulivyo na nguvu, huenda ukakata mbali vya kutosha kutoka kwako, kuhakikisha kwamba uko—uko huru na dhambi, ndipo wewe, kama una nguvu za kutosha, unaweza kukata kuingia katika uponyaji, unaweza kukata kuingia kwenye chochote ambacho Mungu aliahidi, yote yako huko nje. Kama alivyomwambia Yohua, “Kila mahali nyayo za mguu wako zitakapokanyaga, hiyo ni milki.” Inategemea jinsi mkono huo wa imani ulivyo na nguvu unaotumia huo Upanga wa Neno la Mungu.

¹⁰² Loo, ni kweli, alikuwa na vizuizi vingi, bali imani yake haikuwa na kizuizi chochote. Huenda ukawa na baadhi. Nina vingi sana, vizuizi vingi. Lakini kuhusu imani yako, jambo ndilo hilo. Kama huwezi kung’ang’ania, kama utaacha kila kitu kikuzuie. . . Sasa, kimwili, huenda ukajisikia vibaya, kimwili

huenda usijisikie vizuri, na vinginevyo, huenda usijisikie kufa- . . . kwenda kanisani, huenda usijisikie kufanya lolote, bali imani yako haina kizuizi, inaendelea mbele kwa vyovyote vile.

¹⁰³ Labda mchungaji wako alikuombea, akakupaka mafuta, hivyo ndivyo anavyopaswa kufanya, nawe unarudi na kusema, “Mchungaji, sijisikii vizuri zaidi.” Loo, jamani! Wewe si . . . kwanza kabisa hukupaswa kuja. Unaona? Unaona? Unatumia hisia zako. Lakini imani yako, kama una imani . . .

¹⁰⁴ Vema, utasema, “Nitangojea tu mpaka Ndugu Roberts atakapopita hapa, ama Ndugu Branham, ama baadhi ya hao wengine.” Loo, jamani! Hilo silo. Ni imani yako katika Neno la Mungu. Mungu alisema, “Waite wazee wakakupake mafuta na kukuombea. Na kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa yule.”

¹⁰⁵ Iwapo unamwamini Mungu na unaamini hayo maombi, basi endelea mbele kwa vyovyote vile, hakuna kitu kitakachozuia jambo hilo. Unaona? Kwa nini? Una imani, unaamini. Imani haina vizuizi vyovyote.

¹⁰⁶ Loo, lakini mwanamke huyo alikuwa na vizuizi vingi, nawe una vizuizi vingi vya kimwili na vizuizi vya kiroho, bali kama imani yako inamwamini Mungu, hakuna kizuizi chochote kwa imani yako.

Huenda mtu fulani alisema, “Sasa, ngoja kidogo. Sasa, wewe ni Myunani unayemwendea Myahudi.”

“Wewe ni Mbaptisti ukimwendea Mpentekoste.” Mnajua, mambo haya yote.

¹⁰⁷ Baadhi yao huenda walikuwa wakisema, “Sasa, hebu kidogo, Mpenzi, unajua vizuri na vyema ya kwamba siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama hicho, huo ni mhemuko tu. Hivi hatujakuwa na hayo kote katika nyakati? Tumesikia kundi hilo la Wayahudi wanaodai kumwamini Mungu fulani wa kimbinguni, mungu wetu kule chini hekaluni, hukufanyia mengi vile vile, zaidi ya yale angaliweza kufanya. Hakuna kitu kwa hilo.

¹⁰⁸ “Huwaoni watu wetu wakichukuliwa kabisa na udanganyifu kama huo. Tunaiendea sanamu yetu na kuisujudia, na kuiheshimu, na yote *haya*, nasi tunarudi na kuishi maisha ya amani, sikuzote hatuvurugiki kama kundi hilo la watakatifu wanaojibingirisha. Daima wanazozana, *hili, lile*, na *linginelo*, mwajua. Huyu ni mwingine tu . . .” Lakini mnaona . . .

¹⁰⁹ Huenda, mwingine huenda alikuja na kusema, “Sasa, ngoja kidogo. Je, unajua mume wako ni mfanabiashara katika jiji hili? Na huenda mwanao mwenyewe angalikuwa ka—kasisi kwa yule mungu mkuu wa kike *kule* chini, yule mungu wa kike wa Kiyunani. Unajua, ingekuwa—i—ingekuwa vibaya sana. Mume

wako atakufukuza moja kwa moja kutoka nyumbani. Mbona, hupaswi kwenda huko chini, hilo ni jambo la kuchukiza sana.”

¹¹⁰ Na huenda wengine walisimama, wakasema, “Ukishuka uende kule na kitu kama hicho, utakuwa kichekesho cha taifa letu. Kila mtu atakuwa tu *ha-ha* na kukucheka.” Maskini mwanamke huyo alisimama, akasikiliza hayo yote, mwajua.

¹¹¹ Mwajua, na wengine huenda walipanda juu, kuhani wa mungu wake wa kike huenda alipanda juu na kusema, “Sasa, hebu kidogo! Wewe shuka uende kule na uondoe ushirika wako katika kanisa hili.”

¹¹² Loo, alikuwa na vizuizi vingi sana, hapana shaka, bali mwajua, hilo halikumkomesha, alishikilia. Hao, wote huenda walikuwa sahihi, lakini bado kulikuwa na kitu ndani yake, aliamini kwamba alikuwa kwenye njia ifaayo. Aliamini ya kwamba kama Yeye alikuwa ni Mungu hata kidogo, Yeye alikuwa ni Mungu wa kila taifa, kama Yeye alikuwa ni Mungu hata kidogo, Yeye ni Mungu wa maumbile yote, na kama angeweza kumponya Myahudi, angeweza kumponya Mmataifa. Kwa hiyo illeta tofauti gani kama alikuwa Myahudi ama Mmataifa? Alikuwa anaenda Uweponi mwa Mungu. Loo, jamani! Hilo lililishindilia.

¹¹³ Sasa, yeye akapambana na hayo yote, sasa, angalia yale yaliyombidi kupitia, na mambo mengine mengi ya, kama ningalikuwa na wakati ningeweza kuyapitia, mwajua, lakini niseme tu mambo hayo. Naye ilimbidi kupigana na hayo yote, ndipo akafika Kwake, na sasa Yeye amejificha chumbani. Sasa, mlinzi mlangoni akasema, “Hasha, hakuna mtu anayeingia. Yuko mle ndani, lakini amechoka, usimsumbue.”

¹¹⁴ Labda Simoni aliketi mlangoni, mwanafunzi, kasema, “Sasa, ukimfikia, itakubidi kupita juu yangu.” Mwingine, huyu hapa Andrea amesimama nyuma yake, mwingine nyuma yake. Loo, jamani, lakini kwa namna fulani, sijui jinsi alivyofanya jambo hilo, bali alifika Kwake. Mnaona?

¹¹⁵ Ndipo alipofika Kwake, alimwelezea kisa chake, kile alichokuwa nacho niani, binti yake alikuwa mgonjwa. Na sasa angalia sikitiko, hata Yule hasa aliyemjia, Yule ambaye alijua kuwa ni Mungu! Na Yeye—Yeye akasema, “Sijatumwa kwa jamii yako.” Whiu! Hmm! Hiyo ilikuwa ni alama ya jinsi gani! “Nimetumwa kwa watoto wa Mungu, nanyi si kitu ila kundi la mbwa.”

¹¹⁶ Mbona, hilo si lingewalipulia Wapentekoste juu hewani? Loo, jamani, hmm! Loo, “Nimetumwa kwa jamii ya watu ambao wameniamini Mimi. Nimetumwa kwa Wayahudi, watoto, nami sina budi kuwalisha *hao*, si ninyi kundi la mbwa,” akimwita mbwa, kasema Yeye hakutumwa kwake.

¹¹⁷ Lakini mnajua imani, angali alishikilia, aling’ang’ania, mvumilivu. Kwa nini? Alikuwa na imani. Alijua ya kwamba

Huyo alikuwa ni Mungu. Naye alijua ya kwamba kama Yeye angeweza kumponya Myahudi. . . Alimwumba Mmataifa, sawa na vile alivyomwumba Myahudi. Kulikuwa na mahali fulani angeweza kumgusa Yeye. Loo, ndugu, napenda hilo. Endelea tu kugonga. Amina.

¹¹⁸ Bisha. Sasa, tafsiri sahihi ya hilo si “yeye anayebisha,” ni “abishaye.” Yeye aombaye, si kusema, “Bwana,” ama, yeye abishaye, ninii tu [Ndugu Branham anagonga mara moja—Mh.], kisha aondoke. La, wewe endelea tu kusimama pale ukibisha. [Ndugu Branham anabisha mfululizo.] “Bwana, ninataka kuingia, nifungulie.” Jambo ndilo hilo, jambo ndilo hilo. Uh-huh. Kama yule mjane na hakimu dhalimu. Mnaona? Endelea tu kubisha sikuzote.

¹¹⁹ Alikuwa amedhamiria. Imani ilishika kitu fulani, naye akang'ang'ania nacho. Alijua ya kwamba ilimbidi kufika pale, maana labda mmoja wa majirani zake alikuwa na ha—hali ya namna ile ile, mwanamke fulani wa Kiyahudi ambaye alijua alikuwa na binti kama huyo naye akaponywa. Ilimbidi kufika huko, hakukuwa na lingine. Hana budi kufika kule, naye aling'ang'ania, haidhuru kama Yeye alimkataa, “Vema, hiyo ni kweli.”

Kasema, “Enyi kundi la mbwa hata hamstahili hiki Chakula. Sina budi kuwalisha watoto huku.”

¹²⁰ Akasema, “Hiyo ni kweli, Bwana.” Mnaona? Ati nini? Imani, hii inachoma moto, nami natumaini mnaipata, imani daima hutambua Neno kuwa ni kweli. Uh-huh. Hiyo ni kweli. Imani daima huliidhinisha Neno kwa “Amina.” Haidhuru kitu kingine chochote ni nini, Neno daima ni sahihi. Haidhuru kama wanasema, “Siku za miujiza zimepita,” nayo Biblia ilisema, “Yesu Kristo, yeye yule jana, leo, na hata milele,” imani inasema, “*Hiyo ni Kweli.*” Na hiyo ni kweli. Kama wakisema, “Roho Mtakatifu ni kwa ajili ya kundi fulani tu huko nyuma, mia moja na ishirini kwenye Siku ya Pentekoste,” nayo Biblia ilisema, Petro alisema huko Pentekoste, “Ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie,” imani inashikilia hilo. Hakuna mtu anayeweza kuiondoa kwako, umeipata.

“Loo, sijui kama, hakuna mtu, kamwe sikulipokea.”

“Mungu aliliahidi, nami hapa ninalifuatilia.”

“Hiyo ni kwa ajili ya siku nyingine.”

¹²¹ “Ni kwa ajili yangu pia, kwa sababu Kitu fulani ndani yangu kinaniambia ya kwamba Yeye anapenda tu leo hii kadiri alivyowahi kupenda, Yeye ni Mungu yeye yule.” Ndipo unaweza kung'ang'ania na ukae papo hapo, ukibisha, ukitafuta, ukishikilia mpaka Roho Mtakatifu atakaposhuka juu yako. Amina. Sasa, ninajisikia kubarikiwa. Naam, bwana. Amina. Ninajua hiyo ni kweli, nimejaribu, ninajua ni kweli.

¹²² Vema. Imani yake ilishikilia. Jamani! Loo, ninapenda hilo. “Naam,” akasema, “hiyo ni kweli, Bwana, mimi ni mbwa, mimi ni Mmataifa, sistahili yoyote ya baraka hizi, hizo kwa kweli ni mali ya Wayahudi, Wewe ulikuja kwa walio Wako. Ninaamini kila sehemu ya hayo.” Lakini hata hivyo, bado ndani ya moyo wake, hakuumia, hakujisikia vibaya juu yake, alikuwa akiitambua ile Kweli.

¹²³ Sasa, kama Mungu akija awaambie ya kwamba baadhi ya hali baridi za kawaida, kwamba mtaangamia katika dhambi zenu kama mkiendelea hivyo, vema, mngelipuka, jamani, jamani, jamani! Msingeyasikiliza hayo, mngesema, “Huyo ni nabii wa uongo.” Hata hivyo, Neno linakwambia hiyo ni kweli, bali hutasikiliza Neno. Loo, ndugu, ninalipenda.

¹²⁴ Jamani, yeye hakuwa mmea wa tuta. Hakuwa ninii, haikumbidi kunyunyiziwa, chotara kama baadhi ya yale mazao ambayo kizazi hiki kimezaa, ilibidi yadekezwe kila mahali. La. Inambidi kuyachukua . . . na loo, angelichukua kwa njia yoyote ile Yeye aliyompa. Hivyo tu. Alikuwa pale kwa ajili yake, alilitaka. Sio, “Bwana, sasa Wewe—Wewe acha kuzungumza nami namna hiyo, kisha uje nyumbani kwangu.” Hiyo—hiyo haikuwa . . . Yeye alininii—Yeye alitaka tu kumsikia . . . Yeye . . . Alimtaka tu aseme hivyo, hivyo tu, hilo tu ndilo alilotaka kusikia, Yeye tu aseme hivyo.

¹²⁵ Haikumbidi kunyunyiziwa tena, na kudekezwa, na kupapaswa-papaswa na, “Loo, sasa, Mpenzi, unapaswa kuja. Unajua, kama utakuja usiku wa leo, nitaenda pamoja nawe wakati fulani, mahali fulani.” Loo, rehema! “Loo, hebu nikwambie, nitamwomba mchungaji wetu akupatie kiti cha mbele, nami ni—nitakuwa na mahojiano maalum pamoja naye baadaye.” Loo, jamani, kudekeza kitu kama hicho! Huo ni upuuzi wa kichotara.

¹²⁶ “Wote alionipa Baba watakuja Kwangu,” alisema Yesu. “Wala hakuna mtu awezaye kuja, asipovutwa na Baba Yangu.” Pima hilo katika mizani yako wakati mmoja, uone mahali ulipo. Naam, bwana. Unaona, litamulika. Amina. Naam, bwana. Weka Gaiga kwenye hilo uone kitakachotukia. Hiyo ni kweli. Litamulika. Kwa nini? Ni Neno halisi la kweli la Mungu. Yesu alisema, “Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu, asipovutwa na Baba Yangu. Na wote alionipa Baba watakuja.”

¹²⁷ Haikubidi kuwadekeza, na kuwapapasa-papasa, na kuahidi watakuwa na mlolongo wa Makadilaki kama watampokea Roho Mtakatifu, nao wataninii, biashara itanawiri, nao watakuwa na makanisa makubwa zaidi, na minara mirefu zaidi, na wahubiri walioelimika zaidi, na . . . Loo, upuuzi! Ondokeni kwake. Imani inayoshikilia Neno la Mungu, hutumia nguvu za Mungu. Kweli. Ndipo unang’ang’ania.

128 “Mbona, bado sina mlolongo wa Kadilaki, nami nimekuwa hapa pamoja nanyi mwaka mzima, yote niliyo nayo ni mateso mengi.” Loo, ewe punda chotara! Hata hujui baba na mama ni nani. Hivyo ndivyo ilivyo hata hivyo. Jamani, jamani! Naam.

129 Loo, alikubali ile kweli, “Siistahili, Bwana, hiyo ni kweli.” Lakini alisema, nini? “Nipo hapa kwa ajili ya makombo tu. Ni kweli, watoto wanakula, umesema kweli, Bwana, Maneno Yako ni kweli, kila Moja la Hayo, nami sistahili kuketi mezani pamoja na—pamoja na watoto, bila shaka sistahili, bali, Bwana, hebu nikufahamishe jambo fulani, mbwa wako tayari kula makombo yanayoanguka kutoka mezani pa watoto.” Haleluya! Hilo lilimpata.

130 Jinsi ilivyo tofauti siku hizi! Jinsi ilivyo tofauti na sisi watu tunaajiita Wapentekoste! Tusipopata mkate mzima, nao umepakwa siagi, hatuutaki. La, bwana, hatuna uhusiano wowote nao, loo. Loo, jamani! “Ama tupate wote au tusiwe na chochote kabisa,” mnajua jinsi wanavyolisema.

131 Ndugu, alikuwa akitafuta makombo. Akasema, “Bwana, hiyo...loo, Wewe ni...Hiyo ni kweli. Uliyosema ni kweli.” Imani daima hutambua ukweli. Lakini akasema, “Niko hapa kwa ajili ya makombo tu, laiti ningalipata tu makombo! Mimi ni mbwa, lakini mbwa wamejaliwa kula makombo.” Loo, ndugu!

132 Basi kumbukeni, yeye alikuwa Mmataifa, kamwe hakuwa ameona mwujiza. La, bwana, kamwe hakuwa ameona mwujiza, alikuwa ni Mmataifa. Lakini haikumbidi kuonyesha, Haikumbidi kuja, aseme, “Sasa, angalia hapa, ninataka kukuonyesha jambo fulani, ninataka uangalie. Angalia ninii... Angalia hapa, nitaomba kwa dakika moja, angalia Damu ikitiririka kutoka mikononi Mwangu.” Angeweza kufanya hivyo, hakika angeweza.

133 Angeweza kusema, “Ngojeni kidogo, hebu niwaonyeshe mmoja wa miujiza Yangu. Niletene maji kidogo. Unajua, nabii Musa, ambaye Mimi ndiye... Ninachukua mahali pake. Lakini nakwambia, aligeuza bahari ikawa maji kule chini...damu. Unaamini hilo?”

“Ndiyo.”

“Vema, basi nilettee sufuria ya maji hapa, nitakuonyesha ninaweza kufanya jambo lile lile.” Loo, huo ungekuwa ni upuuzi, yeye hakutaka kuona hilo.

134 Alikuwa kama Rahabu yule kahaba, wakati wale wapelelezi walipoenda kuipeleleza nchi naye Rahabu akawaona, hiyo ilikuwa ndiyo nafasi yake ya kwanza aliyokuwa nayo, yeye hakusema, “Aisee, mleteni Yoshua hapa nimwone. Hebu nimwangalie vizuri. Yeye ni jamaa mkubwa mno, mwenye sura nzuri? Je, ana nywele za mawimbi? Vema, unajua, huenda nikamwamini kuwa ndiye kiongozi wa bendi ya Mungu.”

¹³⁵ Hakutaka kumwona Yoshua, hakutaka kuona yoyote ya miujiza yake, alisema, “Nilisikia,” amina, “ya kwamba Mungu yu pamoja nanyi, nami nataka kwenda pamoja nanyi pia.” Amina. Alishikilia. “Sijali yale hao watu wangu wengine wanayofanya, jinsi walivyojizatiti vizuri, jinsi walivyojiimarisha, Mungu amewapa mahali hapa, nami ninataka kuambatana nanyi.” Amina. Aling’ang’ania. Naam, bwana.

Kama vile Rahabu, hivyo ndivyo mwanamke huyu Mmataifa alivyokuwa. Aling’ang’ania, akasema, “Mimi... Mbwa wanaweza kula makombo.”

Yesu akasema, “Kwa msemu huu...” Loo, jamani! Ati nini? Alikuwa ameiendea Karama ya Mungu kwa njia ifaayo.

¹³⁶ Na kama ukimwendea Roho Mtakatifu, Karama ya Mungu, kwa njia ifaayo, si kwamba tu utapata makombo, utapata sahani nzima, iwapo tu utamwendea kwa njia ifaayo. Kuna njia moja tu ya kuliendea, hiyo si kupeleka barua yako kutoka kanisa moja hadi lingine, hiyo si kukimbia kutoka dhehebu moja hadi lingine, hiyo si ya, mnaona, kukariri ile inayoitwa kanuni ya imani, ama, “kanuni ya imani ya mitume.” Si kanuni ya imani ya mitume.

¹³⁷ Na kama utakariri kanuni sahihi ya imani ya mitume, itakuwa sawa, *Matendo* kinakwambia jinsi ya kufanya jambo hilo: “Petro alisema, kwenye Siku ya Pentekoste, akasema, “Tubuni,”” haya basi, “tubuni mkabatizwe, kila mmoja wenu katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.”” Hiyo ndiyo kanuni ya imani, hiyo ndiyo njia ya kufanya jambo hilo. Naam, bwana.

¹³⁸ Alielewa basi, alilielewa vizuri. Alikuwa akiendea hiyo Karama kwa njia ifaayo. Na kama utaiendea vivyo hivyo, “Tubuni mkabatizwe,” basi una hakika ya kumpokea Roho Mtakatifu maana Mungu aliliahidi (Ni kweli kabisa.) kwa Neno lenye mamlaka.

¹³⁹ Unasema, “Mbona, Mtakatifu Christopher *Fulani-wa-fulani* alisema *hivi-na-hivi*, na Dwight Moody mashuhuri...” Watu mashuhuri, sisemi hawakuwa, bali hawana mamlaka. Kama wao ni... Kuna Mamlaka moja tu, na hiyo ni Biblia hii.

¹⁴⁰ Unasema, “Mbona, kanisa la Kiwesley hufanya *hivi*, nao wananyunyizia maji badala ya kubatiza,” mambo haya mengine yote waliyoyavuruga kabisa. Unasema, “Mbona, walikuwa watu mashuhuri.” Sijali, naamini walikuwa hivyo, pia. Ninaamini walikuwa watu mashuhuri, pia, lakini wao ni...hawana mamlaka ya haki ya kufanya hivyo, kwa maana Biblia ilisema, “Yeyote atakayeondoa Neno moja kutoka kwa Hili ama kuongeza lolote Kwake, huyo ataondolewa sehemu yake katika Kitabu cha Uzima.” *Hili* ndilo Neno, *Hili* ni Kweli.

¹⁴¹ “Vema, najua, lakini unaona, tumeelimika, na wachungaji wetu wamefanya *hivi-na-hivi*, wana elimu *kubwa*, nao

wamejifunza Biblia, walisoma historia yote, nao wanadai ya kwamba siku za miujiza zimepita.” Lakini Mungu alisema sivyo, Yesu alisema, “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya; na kazi kubwa zaidi.”

¹⁴² Mtu fulani alisema, “Loo, hakika, tunafanya kazi kubwa zaidi kwa sababu tuna madhehebu makubwa kuliko aliyokuwa nayo Yeye. Tuna ninii kubwa zaidi. . . tuko kote ulimwenguni.” Ngoja kidogo, kabla hamjafanya hivyo, fanyeni kazi alizofanya kwanza, na ndipo mnaweza kufanya kubwa zaidi. Yeye alisema mfanye kazi Zake kwanza, kisha mziendee zilizo kubwa zaidi. Kama utachukua tafsiri yake kutoka kwa ya asili, halikusema, “kubwa zaidi,” ilisema, “nyingi zaidi.” Matendo yale yale na mengi zaidi, kote ulimwenguni, ndipo mmelipata vizuri. Naam. Lakini hilo hapo, neno lisilo na mamlaka.

¹⁴³ Mtu fulani aliniuliza hivi majuzi, akasema, “Mbona, Ndugu Branham, hivi huamini katika toharani?”

Nikasema, “Hakika, ninaamini katika toharani.”

Kasema, “Vema, sawa,” kasema, “hilo ni zuri.” Kasema, “Unajua. . .”

¹⁴⁴ Nikasema, “Lakini siamini ya kwamba ukiisha kufa kasisi fulani akuombe utoke humo, ama mhubiri fulani.” Nikasema, “Ninaamini katika toharani, hakika, kuitakasa nafsi yako, bali tunafanya hivyo sasa. Tunapokosea, hebu na tupige magoti tuwe na toharani, useme, ‘Mungu, nisafishe, toa kitu hicho ndani yangu, nitakase, nioshe, nifanye mpya.’” Ninaamini katika kuitakasa nafsi yangu. Naam, bwana, mimi hufanya hivyo kila siku, niko toharani kila siku basi, unaona, kwa hiyo nikiitakasa tu nafsi yangu kila siku mbele za Mungu.

“Vema,” akasema, “Mtakatifu Andrea, na Mtakatifu *Nanii*, na Mtakatifu Francis, na hawa wengine wote, wanaami- . . .”

Nikasema, “Hilo huenda likawa ni sawa.”

“Nawe unamjua Mtakatifu *Nanii*, Mtakatifu Cecilia, wao. . .”

¹⁴⁵ Nikasema, “Huenda hilo ni sawa, pia, sisemi hivyo.” Vema, unasema. . . Nikasema, “Hiyo ndiyo sababu mna vitabu mia sita mbalimbali vya kutumia, hamjui mahali mnaposimama, lakini hilo ni neno lisilo na mamlaka.” Nikamwambia sikuamini katika kuwaomba watakatifu.

Kasema, “Lakini Mtakatifu *Nanii* alisema. . .”

¹⁴⁶ “Lakini,” nikasema, “Petro alisema, ‘Hakuna mpatanishi mwingine kati ya Mungu na wanadamu, ila Mwanadamu huyo Kristo Yesu.’ Alikuwa na mamlaka, hao mitume walikuwa na mamlaka.”

Tukibishana kuhusu ubatizo, nilisema, “Wao wanasemaje juu yake?” Sawa. “Angalia yale *wao* waliyosema, hayo mengine ni neno lisilo na mamlaka, *Hili* ndilo Neno.”

147 Unapokuwa na Neno la Mungu, kama ninii yetu . . . kama—kama—kama tuna Neno la Mungu na tunajua ya kwamba ni Kweli, tunaweza kung’ang’ania sana, ndugu, na kuingia moja kwa moja ndani kwa sababu Mungu alisema hivyo. Hiyo ndiyo sababu sikuzote nimelitegemea Hilo, wala siingii mimi mwenyewe, ninaenda Yeye anaponiambia. Ninadumu moja kwa moja na Neno Lake, siendi kulia wala kushoto, ninadumu moja kwa moja Nalo, na hiyo ndiyo sababu Yeye analibariki.

148 Kaa Nalo, haidhuru ibilisi anajaribu namna gani kutupa kila kitu mbele yako, aseme, “Utafukuzwa kanisani mwako ukifanya *hivi*.” Dumu Nalo, Mungu aliliahidi, Hilo ni Neno Lake. Amina. Dumu Nalo, ni Neno lenye mamlaka, Neno la Mungu lenye mamlaka. Hiyo ni kweli.

149 Yeye kweli aliliambia Kanisa hilo, “Yeyote mnayeweza kumwondolea dhambi, ameondolewa; mtakayemwekea dhambi. . .” Lakini lilikuwa ni Kanisa la aina gani? Laiti tungeweza kuhubiri juu ya hilo kidogo wakati mmoja,. Vema. Hatutalihubiri sasa.

150 “Kwa msemu huu,” makombo, “loo, nenda kamwone mtoto wako sasa.” Sasa, Yeye kamwe hakwenda kuliombea, Yeye alilisema tu, na hilo tu ndilo alilotaka kujua.

Ninaweza kumwazia akisema, “Asante, Bwana wangu. Jina Lako Takatifu libarikiwe.”

Tukirudi moja kwa moja, hao wakosoaji wote wamesimama mtaani, “Aisee, ulipata nini?”

“Binti yangu ameponywa.”

“Unajuaje? Alikuwa na kifafa nilipoondoka kule juu.”

“Hilo halileti tofauti hata kidogo, nimeupata.”

“Kwa nini?”

“Yeye alisema hivyo.” Amina, amina.

Akakutana na mchungaji wa mungu wake wa kike kule chini, naye akasema, “Mbona, unajua nini? Nimeandika barua yako.”

“Nitakuепushia shida, hata usiniletee, itupe tu motoni, kwa vyovyote vile.”

“Kwa nini?”

151 “Niko njiani, nimetimiziwa haja yangu, binti yangu ameponywa.” Amina. Kumbukeni, yeye alikuwa ndiye Mmataifa wa kwanza ambaye aliwahi kufanyiwa mwujiza, na Yesu Kristo. Naam. Imani hukubali kwamba Neno ni kweli.

Sasa, hatuna budi kuharakisha, maana kutakuwa kumechelewa, wala hatutaki kukaa hapa muda mrefu sana. Loo, linazidi kuwa zuri sasa. Amina.

152 Martha, Mbele za Yesu, pamoja na ndugu aliyekufa, alikuwa amesoma Neno, jinsi yule mwanamke Mshunami alivyomwendea Eliya. Hilo lilikuwa ni Neno la Mungu. Mnaamini hilo? Mnaamini Eliya alikuwa Neno Lake? Biblia ilisema, “Neno la Bwana liliwajia manabii.” Basi Hilo lilikuwa ni Neno la Mungu, kwa hiyo mara tu alipolifikia Neno, alipata faraja. Hiyo ni kweli.

153 Naye Martha, alijua ya kwamba Yesu alikuwa ndiye hilo Neno, naye akalifikia Neno apate faraja. Aling'ang'ania. Labda wakati aliposhuka kwenda barabarani, baadhi yao walisema, “A-ha, sasa amerudi mjini kisiri tangu ndugu yako alipokufa, yule mliyemwamini.” Lakini alishikilia, akaendelea kushuka moja kwa moja.

154 Alipofika Kwake, kamwe hakumkemea, alisema, “Bwana, kama ungalikuwa hapa, ndugu yangu asingalikufa. Lakini hata sasa,” (Loo, ndugu!) “hata sasa, lolote utakalomwomba Mungu, Mungu atakupa.” Huko ni kung'ang'ania, ndugu.

Akasema, “Loo, hakika, ndugu yako atafufuka tena.”

Akasema, “Naam, Bwana, ninaamini hilo, alikuwa mvulana mzuri, atafufuka katika ufufuo wa kiama, siku ya mwisho.”

155 Yesu akasema, “Lakini Mimi ndimi Ufufuo, na Uzima.” Amina. “Yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, hata hivyo ataishi.” Aliona alikuwa aking'ang'ania.

156 Kama vile Eliya alivyomwona yule mwanamke Mshunami, yeye alisema, “Kama vile nafsi yako isivyokufa, na, si—sitakuacha. Nitakaa hapa mpaka nione mapenzi ya Mungu ni nini.”

157 Loo, ndugu, laiti ungalichukua Biblia hiyo na kuketi chini na kuona kama kanuni yako ya imani ni sahihi, iwapo ungaliona tu kama Roho Mtakatifu ni wa kweli, isome tu Biblia nzima, na ung'ang'anie, ushikilie ahadi hiyo utakapoipata. Unaamini katika uponyaji? Shikilia ahadi hiyo. Ng'ang'ania, kuwa Mkristo halisi. Naam, bwana. Hakika, ng'ang'ania.

158 Petro alipokuwa amefundishwa, na baba yake . . . Nitaacha mfululizo wangu wa kawaida wa Maandiko hapa, nitasema tu jambo fulani tena, maana kunachelewa.

159 Petro alipokuwa amesikia, kwa babaye . . . Simoni, hapana shaka yeye na Andrea huko nje kwenye merikebu mara nyingi pamoja na baba yake, yule mzee mwenye mvi alikuwa akifa, kasema, “Mwanangu, sikuzote nimetaka- . . . niliamini ningeishi nipate kumwona Masihi. Lakini kutakuwako na manung'uniko makubwa juu Yake, mwajua, kama tu vile ilivyo daima wakati Mungu anapofanya jambo fulani. Kutakuwako na *hili, lile, linginelo*. Lakini nitakwambia, usichukue ushahidi mwingine wowote ila ushahidi wetu wa Kimaandiko, kwa kuwa Biblia ilisema ya kwamba 'Bwana Mungu wetu atatuondokeshea Nabii,

kama Musa, na huyo Nabii tunapaswa kumsikia.' Nasi tunajua kile Masihi huyo atakachokuwa."

¹⁶⁰ Basi wakati Petro alipoenda kule, kidogo akiwa na shaka, maana ilimbidi Andrea kwenda kumchukua... Na kwa hiyo, alipoenda akamwona, alisema, "Njoo, njoo huku, usiku wa leo, ukamsikilize Yeye dakika chache."

¹⁶¹ Ndipo Petro alipokuja, Mbele Zake, Yeye alisema, "Jina lako ni Simoni, nawe ni mwana wa Yona." Huh! Nena kuhusu kung'ang'ania! Aling'ang'ania sana hata Yesu akasema, "Wewe ni mwamba. Naam, bwana. Kweli utadumu kwenye njia. Nitakupa wewe funguo za Ufalme, na lolote utakalofunga duniani litafungwa; utakalofungua Mbinguni litafunguliwa. Na lolote utakalofungua ama kufunga Mbinguni na dunia-... nitafanya Mbinguni kama unavyofanya duniani." Kung'ang'ania? Ningesema aling'ang'ania. Naam, bwana. Alikuwa na uvumilivu. Naam, bwana. Vema.

¹⁶² Filipo alikuwa amesimama pale naye akaona jambo hilo, aling'ang'ania sana, sana hata akasongamana na mmoja wa marafiki zake wa kimadhehebu na kusema, akamshawishi aje ajionee mwenyewe, kung'ang'ania sana, hakika.

¹⁶³ Yule mwanamke kisimani, alikuwa huko nje, katika sifa mbaya, katika hali mbaya, ndipo siku moja wakati Yesu alipokuja kisimani na kumwona amesimama pale, na kuomba maji anywe, basi alimkemea, kasema, "Mbona, Wewe ni Myahudi, Nawe unaniomba mimi kitu kama hicho?" Kasema, "Mbona, Wewe wajua vizuri sana Wewe, kijana, Myahudi, huna shughuli ya kuniuliza mimi, mwanamke Msamaria, kitu kama hicho. Hatuna uhusiano wowote sisi kwa sisi. Hivi hujui kuna ubaguzi? Kwani umetoka wapi hata hivyo?" Mnaona? "Usiniulize kitu kama hicho."

Akamtazama usoni mwake na kusema, "Lakini kama ungalijua ni Nani uliyekuwa unasema naye, ungeniomba Mimi maji unywe."

¹⁶⁴ Luo, ati kung'ang'ania? Alijua mahali alipokuwa amesimama, pia, sivyo? Baba alikuwa amemtuma huko juu, mwajua. Alikuwa na haja ya kupitia Samaria alipokuja Sikari. Halafu basi, wakati aliposimama pale, nasi tunamwona amesimama pale, aking'ang'ania sana, Yeye hakukubali tusi lake.

Naye akamtazama, Naye akaanza huko... Akasema, "Mbona, tunaabudu kwenye mlima huu, nanyi mnasema huko Yerusalemu." Na mazungumzo yakaendelea.

Akasema, "Nenda, kamwite mume wako."

Akasema, "Vema, sina yeyote. Kwa nini unaniomba kitu kama hicho?"

Akasema, “Ulisema, ulisema kweli. Umekuwa na watano, na yule unayeishi naye sasa si wako.”

¹⁶⁵ Loo, ndugu, hilo lilibadilisha mambo. Akasimama, akasema, “Bwana, naona kwamba Wewe ni nabii. Sasa, hatujakuwa na yeyote wao kwa mamia mengi ya miaka. Lakini tumefundishwa ya kwamba tutampata Masihi, na Masihi huyo atakapokuja, Yeye atakuwa ni Nabii.”

Akasema, “Mimi ninayesema nawe Ndiye.” Loo, akang'ang'ania kwelikweli! Akashikilia.

¹⁶⁶ Sasa, kumbukeni, kama mtu yeyote anajua desturi za kimashariki, mwanamke mwenye sifa hizo hana shughuli kuwaambia wanaume lolote. Hiyo ni kweli. La, bwana, hata hawatamsikiliza. Mwanamke mwenye sifa mbaya, akishuka kuja mtaani, mwenye sifa mbaya, wanaume hawatakuwa na uhusiano wowote naye, hiyo ni kweli, sauti yake si kitu.

¹⁶⁷ Lakini, ndugu, aling'ang'ania kwelikweli, akampata kuhani kisha akawapata wote, alikuwa amekusudia watajua. Akasema, “Angalieni,” kwa maneno mengine, “Yachunguzeni Maandiko yenu, huyo Mtu aliniambia mambo ambayo nimefanya. Haimkini Huyu kuwa ndiye Masihi?” Inyamazishe sauti yake kama ungeweza, usingeweza kufanya hivyo, aling'ang'ania, “Huyo ndiye Masihi. Hiyo hapo nafasi yetu, Huyu Ndiye ambaye tumemngojea, naye Huyu hapo amesimama.”

¹⁶⁸ Na kwa kung'ang'ania kwa dhati sana kwa mwanamke huyo, hata watu mjini waliamini jambo hilo. Hawakusema, “Sasa, wewe njoo uniambie nini. . . Mimi ni nani? Nilitoka wapi?” Hawakuamini hilo, kung'ang'ania kwa mwanamke huyo kulithibitisha ya kwamba Yeye alikuwa ni Masihi. Nayu Biblia ilisema, “Nao watu wa mji huo wakamwamini kwa sababu ya ushuhuda wa huyo mwanamke.” Akashika moto. Loo, jamani!

¹⁶⁹ Ninaweza kumwona maskini mwanamke mmoja huko nje mtaani, naye amefanya kosa, amefanya kila kitu katika kalenda ambacho ni kibaya, na muda si muda mwajua, anayumbayumba akiingia kwenye misheni ndogo mahali fulani, huku amejipodoa na kujipaka rangi za makucha kote usoni mwake, naye ameketi pale akiangalia, akisema, “Mimi sistahili kuwa mahali hapa.”

¹⁷⁰ Muda si muda mwajua Roho Mtakatifu akasema, “Nimekuchagua wewe.” Loo, hebu komesha ushuhuda wake wakati mmoja! Loo, ndugu, yeye anang'ang'ania sana! Huenda asininii. . . Mtu wa bima anakuja mlangoni, anainamisha kichwa chake chini kwa aibu, anaenda mlangoni, kesho yake anaweza kutoa ushuhuda ambao utatikisa viezekeo kutoka juu ya nyumba. Naam. . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Yeye anang'ang'ania, ndugu, anajua amegusa Kitu kifaacho. Jambo ndilo hilo, ng'ang'ania, usikate tamaa.

¹⁷¹ Yohana Mbatizaji aling'ang'ania, alijua. Inanikumbusha juu ya Tommy Nickel. Sidhani yuko hapa pamoja nasi, sivyo? Yeye ni

maskini ndugu mzuri, ninaweza tu kumjivunia sana sasa. Naye alikuwa pamoja nasi hivi majuzi usiku.

¹⁷² Nilikuwa na ono la kuwa Utukufuni na kurudi, wala Tommy hakulichezea, hata katika gazeti hilo la kimataifa, aliliweka mle jinsi tu lilivyokuwa. Wengi wenu mlisoma. Na ile sehemu ndogo chini ya kurasa, mliisoma hiyo? Alizungumza juu ya huduma ya siku zilizopita, na kusema ya kwamba Mungu alikuwa hata amenitumia mara nyingi, na kuthibitisha kwa ushahidi, ya kwamba Yeye amewafufua wafu, na kile walichokuwa nacho, ushuhuda, tunao, wa huko chini Meksiko usiku mmoja si muda mrefu uliopita.

¹⁷³ Nilikuwa na mkutano katika Jiji la Meksiko, nasi tulikuwa kwenye uwanja huo mkubwa wa michezo huko nje, na maelfu ya watu walikuwa wamesimama, nami nilikuwa tu na yapata siku tatu au nne usiku. Na mmoja . . . Usiku wa pili pale . . . Usiku wa kwanza, niliwafundisha tu watu. Wote walikuwa wamesimama pale, maskini, hawana viti vya kukalia, wamesimama tu moja kwa moja katikati ya uwanja, na mahali fulani karibu watu elfu ishirini ama thelathini. Ndipo nikaanza kuwazungumzia juu ya Bwana Yesu, na kuhusu neema Yake kuu, na rehema Zake kwa watu, na kuwashuhudia yale aliyokuwa amefanya.

¹⁷⁴ Ndipo usiku wa pili tukashuka kwenda kuwaombea. Akaja mzee mmoja wa Kimeksiko kupitia madhabahuni, kipofu, hakuwa amevaa viatu, maskini miguu yake iliyochakaa na kadhalika, na jinsi alivyoonekana, niliwazia juu yake, nami nikawazia . . .

¹⁷⁵ Hapa si muda mrefu uliopita wakati bunduki hii iliponilipukia . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . ? . . . Ilichokuwa, ni Winchester iliyobadilishwa ikawa Weatherby Magnum. Nafikiri mtu aliyenipa hiyo ameketi papa hapa sasa. Naye . . .

¹⁷⁶ Sikuzote nilitaka Weatherby Magnum. Kamwe sichezi gofu, na kutoka nje pamoja na kundi hilo la wanawake na kadhalika huko nje, Mungu alinipa burudani: kuwinda na kuvua samaki. Na daima nilipenda Weatherby Magnum, ni maridadi, nami nilitaka moja, lakini inagharimu pesa nyingi sana. Nina marafiki wangeninunulia hiyo, kama nilivyo sema hivi majuzi usiku, “Ningewezaje kumwacha mtu aninunulie Weatherby Magnum ya mamia ya dola, huku nikiwa na marafiki wamishenari wasio hata na viatu miguuni mwao?” La, bwana.

¹⁷⁷ Na maskini hao Wameksiko huko chini, hawana kitu, maskini miguu iliyochakaa, huku wamevaa koti kuukuu, na lote limechakaa, na labda kamwe hakupata chakula kizuri maishani mwake, huku ana watoto wanne au watano nyumbani, na halafu mbali na hayo alikuwa kipofu. Ningempa koti langu, ningempa viatu vyangu, chochote kile, alikuwa mtu mkubwa zaidi, ila nilimpa upendo wangu. Nikamkumbatia na

kumwomba, ndipo Mungu akayafumbua macho yake papo hapo jukwaani, akakimbia huku na huko akipiga mayowe.

¹⁷⁸ Maskini mwanamke wa Kimeksiko . . . Aliyeingia Meksiko, kote mjini, kesho yake kulikuwa na lundo la nguo pana kuliko *hili* hapa, zimelundikwa juu *hivi*, la shali kuukuu tu na kofia, watu wakijaribu kuponywa.

¹⁷⁹ Maskini mwanamke mmoja wa Kimeksiko asubuhi hiyo alimpeleka mtoto wake mchanga kwa daktari, alikuwa anapumua kwa shida tu, nimonia iliyasonga mapafu yake. Alipokuwa ofisini, huyo mtoto mchanga akakoma kupumua, daktari alimtia Kipumulizi, asingeweza kumrudisha, alikuwa amekufa, saa tatu asubuhi hiyo. Akamwambia mama, kasema, “Tunamrudisha . . .”

¹⁸⁰ Akasema, “La, nitamhifadhi huyu mtoto mchanga.” Naye akamweka mikononi mwake akakimbia nyumbani, akaenda kwa jirani yake na kusema, “Si ulisema ya kwamba mmoja wa watu wetu alifunguliwa macho jana usiku, kule?” Alikuwa ni Mkatoliki, kasema, “Hivi, hukusema mmoja wa watu wetu alifunguliwa macho kwenye jukwaa lile?” Akasema, “Ninampeleka mtoto wangu.”

¹⁸¹ Huyo akaenda pamoja na mtoto huyo kwenye mvua, alienda saa tatu na nusu, saa nne asubuhi hiyo, na kusimama huko hadi saa nne na nusu usiku huo, kabla sijaingia. Huku kukinyesha, maskini hao Wameksiko wamesimama kule, hao wanawake, nywele zao zimeshuka usoni mwao, wamesimama pale kwenye mvua hiyo, ikiwaangukia usoni mwao.

¹⁸² Ndugu Jack Moore, na wengi wa hao ndugu, tukashuka, kulikuwa na watu wengi sana karibu na uwanja huo iliwabidi kunichukua, na kunipandisha ngazi upande wa nje, kisha wakanifungia kamba mikononi mwangu, na kunishusha chini, nipate kufika jukwaani nyuma yake, watu wengi sana wamezunguka.

¹⁸³ Ndipo nikapanda pale na kuanza kuzungumza. Nilipoanza tu kuzungumza, ndipo, nikasikia vurugu mbaya sana upande wangu wa kulia, nikawaza, “Ni kitu gani hicho?” Ndipo nikajaribu kuhubiri, na kukawa na vurugu kubwa sana tena.

¹⁸⁴ Ndipo Billy akanijia, mvulana wangu, akasema, “Baba, nilimpa Ndugu Espinoza hizo kadi za maombi, naye akazisambaza . . .” Sijui, nilimwita “Mañana,” alikuwa mwenda pole sana. Nami . . . Kasema, “Alizisambaza . . . Naye alisambaza kadi za maombi, naye maskini mwanamke yule kule anataka kadi ya maombi kwa ajili ya mtoto wake aliyekufa.” Akasema, “Baba, amesimama hapa siku nzima kwenye mvua hiyo.”

¹⁸⁵ Kasema, “Kamwe hatuwezi kumshikilia.” Kasema, “Tuna karibu mabawabu mia moja na hamsini, mia mbili wamesimama pale, naye anapenya tu na kuwapita moja kwa moja.” Kisha

kasema, “Tumemtupa nje ya jukwaa mara tatu ama nne.” Kisha kasema, “Hatuwezi kufanya lolote naye.”

¹⁸⁶ Nikasema, “Ndugu Moore, nenda kule ukamwombe, yeye hajui nani ni nani, endelea tu.” Maskini mwanamke wa Kimeksiko, mimi. . . Alikuwa maskini mwanamke mzuri, mrembo, yapata, maskini jamaa mdogo, na alionekana kuwa na umri wa kama miaka ishirini na mitano, labda mtoto wake wa kwanza. Na kwa hiyo, Ndugu Jack akaanza kwenda pale.

¹⁸⁷ Nami nikasema, “Nilikuwa nikizungumza juu ya Bwana wetu,” ndipo nikaangalia nje, na nikaona maskini mtoto mchanga wa Kimeksiko, mwenye uso mweusi, amesimama mbele yangu, bila meno, akicheza tu na kucheka. Ni—nikaangalia tena, nikasema, “Ngoja kidogo, Ndugu Moore. Mwambie amlete huyo mtoto mchanga hapa.”

¹⁸⁸ Nao wakafungua mstari. Wakati ninii. . . Ndugu Espinoza, wengi wenu ndugu mnamjua, ninyi ndugu wa Assembly of God. Alikuwa. . . Huko ndiko anakotoka. Wakafanya. . . wakaufungua mstari. Huyu hapa maskini mwanamke huyu akaja mbio pale juu, akapiga magoti, akisema, “Padre! Padre!”

Nikasema, “Simama, simama.” Naye alikuwa na shanga mkononi mwake, nikasema, “Ziweke kando tu.”

Nikasema, “Kuna nini?”

¹⁸⁹ Ndugu Espinoza akatafasiri, mtoto wake alikuwa amekufa, naye alikuwa amesimama pale akilia, machozi, macho yake madogo yamevimba, maskini mama. Alikuwa amemlaza chini ya blanketi ndogo, blanketi ndogo ya samawati ikining’inia chini, huyo hapo maskini mtoto mchanga aliyekufa, alikuwa amekakamaa, angeweza kuona mikono yake midogo na kadhalika ilikuwa imelala, imekakamaa, alikuwa amekufa tangu asubuhi hiyo.

Nikasema, “Sasa, Ndugu Espinoza, usifasiri hili,” nikasema, “ni ono ambalo ndio kwanza nione.”

Akasema, “Ati nini?”

Nikasema, “Ono. Usiseme chochote. Acha niombe.”

¹⁹⁰ Nikasema, “Baba wa Mbinguni, si—sijui hili linamaanisha nini, lakini nilikuwa nikiangalia huko nje, na mbele ya macho yangu akaja m—mtoto mdogo aliyekana kuwa yapata ukubwa huu.” Nikasema, “Nitaweka mikono yangu juu ya maskini mwili wake uliokufa.” Na yapata wakati huo akaanza kurusha mateke na kupiga mayowe, kwa nguvu alivyoweza, namna *hiyo*. Nikasema, “Ndugu Espinoza, nenda kwa daktari wake, upate taarifa iliyoandikwa.” Akafanya hivyo.

¹⁹¹ Kwa nini? Aling’ang’ania. Kwa nini? Hakujali yale kanisa lilivyosema, kama alifukuzwa, jinsi ilivyokuwa. Kama kipofu angeweza kufunguliwa macho, mtoto wake mchanga. . . Hakuna mtu angaliweza kuyarejesha macho ya kipofu, mtu yeyote

anajua hilo. Kama vile, hata kwa Mafarisayo ilisemwa, “Ni nani angeweza kuyarejesha macho ya kipofu, isipokuwa Mungu peke yake?” Hakuna mtu angeweza kufanya hivyo, naye alijua hilo, naye alijua kama Mungu alikuwa hapa duniani katika nguvu za kutosha kuyafungua macho ya kipofu, alikuwa ni Mungu yeye yule ambaye angeweza kuwafufua wafu, bado.

¹⁹² Aling'ang'ania, alikaa siku nzima. Huku wazishi wakimtafuta mtoto wake mchanga, alikaa siku nzima haidhuru, mabawabu wakijaribu kumzuia asiingie mstarini, naye akakaa kwa vyovyote vile, alikataliwa kwa kila njia, lakini akakaa. Kwa nini? Aling'ang'ania. Kwa nini? Imani ilishikilia. Imani ilisema, “Ndivyo ilivyo.” Nayo Imani haijui magumu, imani haijui kushindwa. Na unapokuwa na imani, una uvumilivu.

Na tuombe kwa dakika moja. Ni wangapi wanaotaka uvumilivu?

¹⁹³ Baba yetu wa Mbinguni, ninaamini, Bwana, kwa moyo wangu wote, ya kwamba ikiwa watu wangalitambua tu... Ninaamini wao ni watu wazuri, ninaamini hao ni watu Wako, ninajua ndivyo walivyo, wanakupenda, wamepita kutoka mautini kuingia Uzimani, bali moja kwa moja niani mwao kuna Shetani, wakati wote, akijaribu kuwanukulia vibaya jambo fulani, akijaribu ku—kuondoa kwenye Neno la Mungu. Ninaomba, Baba, ya kwamba Wewe utamkemea. Tujalie, Mungu. Jalia Roho Wako Mtakatifu aje juu ya kusanyiko hili, sasa hivi.

¹⁹⁴ Wao, hapana shaka, ya kwamba sehemu kubwa ya watu hawa humu ndani, leo, wameuhisi Uwepo Wako, wanaamini, lakini hebu watambue ya kwamba wana mzuiaji pia, na huyo ni adui, huenda akanena kupitia marafiki wa thamani, bali hata hivyo Neno Lako ni lile lile. Wewe—wewe... Ungewezaje kumfufua huyo mtoto mchanga aliyekufa kwa ajili ya mwanamke huyo wa Kimeksiko, kwa sababu alikuwa na imani, wala usimfufue mtoto wa mtu mwingine? Ungewezaje kumponya kipofu ambaye hangeweza kuona, isipokuwa Wewe ungemponya kipofu mwingine? Lakini jambo ni kwamba, wengi wao wamesimamishwa.

¹⁹⁵ Baadhi yao wana uvumilivu, wanaendelea mbele tu kwa vyovyote vile, haidhuru ni nini, kama maskini yule mwanamke Msirofoinike tuliyenena habari zake alasiri ya leo, aliyesimama mbele Zako. Ulimwambia tu, “Nenda zako, ibilisi amemwacha.” Hayo tu ndiyo aliyotaka kujua.

¹⁹⁶ Sasa, haikubidi kuja miongoni mwetu kusema jambo hilo sasa, Baba, kwa sababu tayari umelisema, “Lolote mtakalo, mkisali, aminini tu mnayapokea, nayo yatakuwa yenu.” Tunajua hilo ni Neno Lako. Sasa, kama tukiomba lolote, basi tunapaswa kuwa na subira baada ya hilo, tunapaswa kujua ya kwamba

ni yetu, Wewe ulitupa, huwezi kusema uongo, Wewe ni Mungu. Kama ukiwapa wengine, kwa nini usitupe sisi?

¹⁹⁷ Ndipo tunaomba, tutapokea, Wewe ulisema hivyo, “Bisheni, nanyi mtafunguliwa; tafuteni, mtapata; ombeni, nanyi mtapewa.” Vema, Mungu, umetupa ahadi baada ya ahadi, “Iwapo mahali popote wawili au zaidi wamekusanyika kwa Jina Langu, na kuomba lolote, watapewa.” Sasa, Wewe uliahidi kwamba, “Walipo wawili watatu wamekusanyika, haidhuru mkutano ni mdogo jinsi gani, nitakuwa katikati yao.” Sasa, Wewe uliahidi jambo hilo, Bwana, hiyo—hiyo ni ahadi Yako Mwenyewe, hilo ni Neno Lako Mwenyewe, ninaliamini.

¹⁹⁸ Ninaamini kwamba, kama tu vile ulivyokuwa umesimama papa hapa, mbele zetu leo, ukashuka kwenye ushoroba wa Mbinguni na kutembea hapa, na kusema, “Niko katikati yenu kwa sababu mmekusanyika pamoja.” Vema, imani yangu inaniambia Wewe upo hapa haidhuru, kwa hiyo Wewe—Wewe uko hapa kama tu vile ungekuwa kama tungeisikia Sauti Yako inayosikika, Hii *hapa* Sauti Yako kwenye karatasi, Ahadi Yako, Nayo ni yetu. Umelilinda Neno hili lililobarikiwa kote katika umwagikaji wa damu, kote katika nyakati, bali lingali linadumu, maana Wewe ulisema Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Lako halitapita.

¹⁹⁹ Ninaomba, Baba, sasa, ya kwamba watu wataelewa ya kwamba Neno Lako ndivyo lilivyo. Ni Mungu, na Yuko miongoni mwetu. Yuko hapa sasa, Mungu aliye hai aliye na Neno lililo hai kumjulisha kila mtu kwa midomo ya mhubiri, kwa midomo ya—ya nabii, kwa midomo ya mwalimu, kwa midomo ya mmishenari, mbona, Wewe uko hapa, Mungu, nasi tunasikia na tunajua ndivyo ilivyo, ndipo tukakuhisi Wewe.

²⁰⁰ Nasi tunaangalia nyuma na kuona ambapo wakati mmoja tulikatwa kutoka kwenye do—donge gumu la dhambi, na sasa tumeinuliwa. Ambapo baraka haziwezi kutujia *kule*, sasa tunazo. Wakati mmoja tulikuwa vipofu, sasa tunaweza kuona; wakati mmoja tulikuwa tumekufa ganzi, sasa tuna hisia; wakati mmoja tulikuwa tumekufa, sasa tuko hai. Arabuni ya chochote tunachotamani, vitu vyote ni vyetu. Tunaambiwa ya kwamba, katika Biblia, ya kwamba sasa tunamiliki vitu vyote, na vitu vyote ni vyetu.

²⁰¹ Wabariki watu Wako, alasiri ya leo, Baba. Kama kuna mwenye dhambi hapa, Baba, ninaomba ya kwamba Wewe uwaokoe sasa hivi. Jalia waje, moyoni mwao, jalia moyo huo uwe ndio madhabahu ya mahali nafsi yao inapotulia, na jalia waweke kutokuamini kwao juu ya madhabahu ya moyo wao na kusema, “Mungu, tangu leo hii na kuendelea, nitakuamini Wewe.”

²⁰² Na huku tumeinamisha vichwa vyetu, na katika maombi, sijui ni wangapi hapa ndani wanaojisikia hivyo, “Bwana, ondoa kutokuamini moyoni mwangu.” Huenda ukawa mfuasi wa

kanisa, huenda ukawa mwaminifu, lakini bado kuna baadhi ya Neno unalosema, “Nina shaka kuwa ndivyo lilivyo,” wewe ungali ni mwenye dhambi.

²⁰³ Kama kueleweka vibaya kidogo kwa Neno la Mungu kwa Hawa kulisababisha mauti haya yote, huzuni, makaburi, magonjwa, uzee . . . Hiyo ni kwa sababu tu . . . sio . . . Mengi sana yalikuwa ni kweli, lakini ninii tu . . . jambo moja dogo tu halikuwa sahihi, naye Hawa akaamini hilo. Huenda ukaamini sehemu tisini na tisa na tisini na tisa ya milioni ya Biblia, na huko kutokuamini moja katika milioni moja, ungali ni mwenye dhambi. Hilo moja liliwaondosha watu kutoka Edeni, hiyo moja juu ya milioni moja haitakuruhusu kurudi ndani tena. Unajua kama moja juu ya milioni moja iliwaondoa, moja juu ya milioni moja haitakuruhusu kurudi baada ya adhabu kama hiyo ya mateso kulipwa.

²⁰⁴ Hivi hutaamini sasa kwa moyo wako wote? Inua mkono wako na useme, “Mungu, unirehemu,” kama unataka kuamini namna hiyo. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Anaona- . . .

²⁰⁵ Kuwa mwaminifu sasa. Haikubidi kuja hapa karibu na madhabahu, Yesu alisema, “Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele.” Hilo latosha. Ama unaamini au huamini. Kama unaamini hilo kwa moyo wako wote, umepita kutoka mautini kuingia Uzimani. Sasa uko katika msafara unaokua, uko kwenye uwanja unaofaa sasa, unaweza kuendelea kuinuka, kutoka kuhesabiwa haki, hata utakaso, hata kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu, kuendelea kuingia katika kutukuzwa. “Kwa kuwa hakuna mtu angaliweza kuinua mkono wake, isipokuwa Baba Yangu alimwita. Na wote alionipa Baba watakuja. Na wale aliotangulia kuwajua amewaita, na wale aliowaita amewahesabia haki, na wale aliowahesabia haki, amewatukuza.” Ninanukuu Maandiko, Neno Lake. Hiyo ni kweli.

²⁰⁶ Liamini sasa, upate Uzima wa Milele. Amini uishi; litilie shaka: ufe. Kwa hiyo pata Uzima wa Milele na umwamini Bwana Yesu Kristo. Popote ulipoinulia mkono wako . . .

[Dada mmoja ananena kwa lugha na kufasiri—Mh.]

²⁰⁷ Amina. Iweni na kicho, kila mtu sasa. Ninii tu, Jina la Bwana libarikiwe. Mwamini Yeye kwa moyo wako wote. Wakati unapofanya maamuzi yako moyoni mwako baada ya hayo, amini kwa moyo wako wote sasa, ungama makosa yako yote, ndipo unaweza kushikilia.

²⁰⁸ Wengi hapa huenda wakasema, “Sielewi hilo.” Kwa nini? Aliifasiri katika Kiingereza dhahiri. Hakika unaamini Biblia, Yeye aliahidi hilo, ya kwamba angemwaga Roho Wake, “Amri ingekuwa juu ya amri; na kanuni juu ya kanuni; hapa kidogo na pale kidogo. Shikilia yaliyo mema. Kwa kuwa kwa midomo ya wageni na kwa lugha nyingine nitasema na watu hawa.

Na hii ndiyo sabato.” “Lakini kwa hayo yote, wasingesikia na kugeuka, masikio mazito.” Mwamini Yeye, ng’ang’ania, mkubali sasa, mwamini Mungu.

²⁰⁹ Toka hapa uende kanisani mwako, nenda, ukamwambie mchungaji wako ya kwamba umemkubali Kristo. Kanisa, kanisa la Injili yote katika ujirani wako, popote pale, nenda ukawaambie umemkubali Kristo. Mwombe mchungaji wako akusaidie, akuongoze zaidi katika Ufalme. Wengi wenu... Ni wangapi wanaoamini ya kwamba Kristo anakusamehe dhambi zako? Inua mkono wako. Huko ni kutokuamini kwako. Mungu awabariki. Asanteni.

²¹⁰ Sasa, badala wa kuitisha mstari wa maombi, nitasimama hapa na kumwomba Roho Mtakatifu awaite watu kutoka kwenye kusanyiko hilo. Sasa, iweni na kicho kabisa, tafadhali, kwa dakika zetu chache zijazo mnapoketi tu, na mwe na kicho kabisa. Sioni mtu mmoja katika jengo hili, wakati huu, ninayemjua. Hakuna mtu ninayemjua ninayeweza kumwona. Lakini sasa hivi nimezungumza nanyi.

²¹¹ Hivi huyu si ni Bw. Sims kutoka Zion anayeniangalia, papa hapa? La, siye. La, naona siye. Ninataka tu kuwa mkweli na kujua kama kulikuwa na... Hakuna mtu hapa ninayemfahamu.

²¹² Mnaamini ya kwamba Kanisa linaumbika katika hali fulani? Jinsi ambavyo Luther alikuwa na njia pana, kumkubali tu Kristo, katika uchache kikaja kipimo cha Kimethodisti, Wapentekoste walikuja zaidi katika uchache, kanisa likifanana zaidi na Kristo, zaidi kama Kristo, na nguvu za kuishi, na sasa Wapentekoste hawana budi kujichonga wapate kupokea lile Jiwe la Kichwa, halina budi kuchongwa sana hata hakutakuwako na sauti ya nyundo, wala mlilo wa dhehebu. Tayari limekatwa. Ni mpango wa Mungu. Roho Mtakatifu hulichonga katika hali hiyo. Wewe amini.

²¹³ Yesu aliahidi katika siku za mwisho kazi alizofanya zingefanywa pia. Nilinukuu Waebrania 4:12 muda mfupi uliopita: “Neno la Mungu,” Hilo lilikuwa ni Kristo, “Ni Mtambuzi wa mawazo ya moyo.” Wakati alipokuwa hapa duniani, aliyatambua mawazo yao na shida zilizokuwako mioyoni mwao, na kuthibitisha jambo hilo. Hakika, kama angekufanyia hivyo alasiri ya leo, usingeweza kuondoka hapa ukiwa asiyeamini. Je, ungeng’ang’ania kama Yeye angekuita?

²¹⁴ Ni wangapi walio wagonjwa humu chumbani? Inueni mikono yenu, huku vichwa vyenu vimeinamishwa, semeni, “Ninataka Mungu anikumbuke katika maombi,” kote kote, kila mahali. Ni wangapi wanaojua ya kwamba mimi ni mgeni kwenu? Inueni mikono yenu, mnaojua ya kwamba mimi ni mgeni kwenu? Ni kila mahali tu. Sasa, iweni na kicho, ombeni kwa dakika moja tu.

²¹⁵ Sasa ninaamini katika nini? Kama Samsoni alivyofanya, alinyosha mkono pale na kugusa hivyo vishungi. Nilipokuwa

nimesimama hapa nikijiandaa kusema, “Acheni watu wapite tu, nao hawa, wahudumu hapa chini wawawekee mikono,” kitu fulani kilinigusa, nikaona ono likisogea juu ya kusanyiko, basi ninajua vishungi hivyo vingali viko, ahadi Yake ingali hapa. Sasa, ninyi ombeni muone kama Yeye si Mungu yeye yule. Basi kama Yeye yuko hapa miongoni mwetu alasiri ya leo, hivi huwezi kushikilia kwa imani yako kumwamini Mungu? Amina.

²¹⁶ Sasa, ombeni tu, mwombeni Mungu awabariki. Fanyeni kama yule mwanamke aliyegusa upindo wa vazi Lake, angalieni jinsi alivyoshikilia, aliwazia, “Kama nikiweza tu kugusa vazi Lake, nitapona. Ninaamini. Ninaamini jambo hilo, ya kwamba Mtu Huyo ndiye Kweli. Haidhuru makuhani wanasema nini, ninaamini ya kwamba Yeye ni yule Nabii wa Galilaya, nami ninaamini hilo.” Naye akasema, “Kama nikiweza kugusa vazi Lake, nitakuwa mzima.”

²¹⁷ Sasa, Yeye angali ni Kuhani Mkuu yeye yule, Biblia ilisema hivyo, anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu. Kama wewe ni mgonjwa sana, sana sasa, kwa nini usininii tu, kwa imani, upasue kupita vizuizi hivyo vya sauti vya ulimwengu, hivyo vizuizi vya sauti vinavyosema, “Hakuna kitu kama hicho. Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama hicho.” Hivi hutapasua kupita hapo ambapo unaweza kuwa huru na kugusa vazi Lake? Na kama Yeye aliahidi, katika Biblia, ya kwamba tungefanya jambo lile lile alilofanya, nami nimewaletea Ujumbe wa kweli kwamba Yeye ni yeye yule, basi mwacheni aufanyie kazi, Yeye aliahidi jambo hilo.

²¹⁸ Kama vile tu yule mwanamke Msirofoinike, ninasimama hapa alasiri ya leo kwa sababu Yeye aliahidi jambo hilo. Nawe uketiye hapo, Yeye aliahidi jambo hilo, wala usiache ibilisi yeyote wala shaka ikuzuie, naye atalijalia, atasua moja kwa moja kupitia vizuizi hivyo na kukuchukua. Wewe amini.

²¹⁹ Kama Bwana angesema nami na kuniambia, juu ya kundi la wageni, jambo fulani unalojua, lingekuwa ni thibitisho muhimu sana, thibitisho la Biblia ya kwamba Yeye yuko hapa pamoja nanyi. Basi ungeweza kwenda nyumbani na kung'ang'ania, ukisema, “Mungu asifiwe”? Ungeweza kufanya kama maskini yule mwanamke Msirofoinike? Alijua alikuwa akirudi, akamkute mtoto huyo mchanga yuko sawa, naam, bwana, alijua ingekuwa hivyo. Iweni tu na imani, aminini sasa.

²²⁰ Sikuwa ninakusudia kufanya jambo hili, nilihubiri juu ya jambo lingine, mnaona. Nilikuwa nikitaka kufanya wito wa madhabahuni, ndipo nilipofanya wito mfupi wa madhabahuni, basi jambo fulani likahamia kwenye hili. Hebu na tuanzia upande wa pili, siwezi kupata ma—mahali pale pamoja katika—katika jengo, sina budi kuanzia upande mmoja, nitaanzia mkono wangu wa kulia na kwenda upande wa kushoto. Sasa, mna wakati? Semeni, “Amina.” [Kusanyiko linasema,

“Amina.”—Mh.] Vema, basi tulieni kwa dakika moja tu, kila mtu, msisogeesogee, iweni tu na kicho, mnaona. Mnatinii. . . ina—inasumbua, mnaona, wakati mnaponinii. . .

²²¹ Sasa, mtu fulani huku na huku kwenye safu hizi humu ndani mahali fulani, wewe amini tu kwa moyo wako wote na kusema, “Bwana, kweli ninaamini kwa yote yaliyo ndani yangu. Ninaamini ya kwamba Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, yupo hapa. Ninaamini ya kwamba Mungu alifanya ahadi, na Mungu atafanya yale hasa aliyohadi.”

²²² Mtu huyo aliyeketi hapa, akiniangalia moja kwa moja, aliyeketi yapata mtu wa pili, amevaa suti ya hudhurungi, anasumbuliwa na shida ya jicho. Sikujui, hatufahamiani. Huenda unanijua mimi, sikujui mimi. Hiyo ni kweli, sivyo? Huenda mtu fulani akasema, “Mtu huyo amevaa miwani.” Hiyo siyo shida yake, ni shida kweli, bali yeye ni mtu mwenye umri wa kutosha kuvaa miwani, ni uvimbe kwenye jicho lake. Hiyo ni kweli. Uko kwenye jicho lako la kulia. Hiyo ni kweli. Wewe ni mfuasi wa Kanisa la Filadelfia. Hiyo ni kweli. Wewe amini, na uvimbe huo utaliacha jicho lako. Sasa, kama hiyo ni kweli, yale yaliyosemwa, inua mkono wako.

Aligusa nini? Yeye yule anayekufanya ulie, na kumsifu Mungu, na kupaza sauti. Unaona? Huyo Ndiye, Yeye yule.

²²³ Moja kwa moja nyuma yake, kwa kuwa huyo roho wa kupofusha alikuwa pale, moja kwa moja nyuma yake kuna mwanamke anayeniangalia, hebu tuone, yapata moja, mbili, tatu, nne, ameketi mle ndani, ana shida ya macho pia. Ataamini kwa moyo wake wote, kitu hicho kitamwacha. Hiyo ni kweli.

²²⁴ Mama anayeketi moja kwa moja huko nyuma, pia akiwa na ugonjwa huo wa kibofu, utaamini ya kwamba Mungu atakuponya, na ugonjwa wa kibofu? Amevaa miwani, amevaa gauni la waridi. Jambo ndilo hilo. Hatufahamiani. Hiyo ni kweli, Mama? Kama mambo hayo ni kweli, inua mikono yako. Umekuacha, imani yako imekuponya.

Mwaminini Mungu. Vipi kuhusu mtu fulani katika marefu haya hapa ndani? Mnaamini? Kuwa tu na imani, hivyo tu ndivyo inavyokupasa kufanya.

²²⁵ Mama huyu aliyeketi papa hapa, mwenye maua kwenye kofia yake, aliyeketi moja kwa moja hapo nyuma akiwa na yabisi kavu, kama unaamini kwa moyo wako wote. . . Naam, wewe, Mama, naam. Kidogo nywele zinaingia mvi, huku amevaa nguo nyeupe. Vema, wewe, ulielekeza kidole chako chini. Imekuacha. Mimi ni mgeni kwako, sikujui, bali Kristo anakujua. Hiyo ilikuwa ni kweli, sivyo? Vema.

Mwaminini Mungu. Mnamwamini Yeye sasa?

²²⁶ Mtu huyo aliyeketi huko nyuma kabisa, hivi hamwoni ile Nuru juu yake? Anamwombea mtu fulani, si yeye, anamwombea

mwanamke fulani, ni mke wake, yeye ana shinikizo la chini la damu. Jina lake ni Bw. Mark. Amini, Bwana. Simjui mtu huyo, sijawahi kumwona maishani mwangu, Mungu anajua hiyo ni kweli. Kama ndivyo ilivyo, Bwana, inua mkono wako. Amini kwa moyo wako wote, itatendeka.

Unaamini? Vipi kuhusu upande huu? Vipi kuhusu baadhi yenu nyote? Aminini.

²²⁷ Ninamwona mama mweusi ameketi papa hapa chini. Kwa kweli si yeye, naam, anamwombea mtu fulani aliyemleta hapa, alienda hospitalini akamchukua mtu fulani. Ni yule mtu aliyeketi mwishoni. Mtu huyo kweli hajui ana shida gani, lakini Mungu asipomponya hana budi kufa. Ulimleta, hii hospitali hapa. Hiyo ni kweli. Kwa namna fulani hata iliumiza akili yake. Hiyo ni kweli, ni kweli.

²²⁸ Nawe, kwamba uniamini mimi kuwa nabii wa Mungu: hatufahamiani, hiyo ni kweli? Wewe ni mgeni tu, umekuja humu ndani. Vema. Kama unaamini kwa moyo wako wote, una jamba unalotaka liombewe, pia. Hilo ni kivimbe, na kivimbe hicho kiko kwenye mguu wako wa kulia. Hiyo ni kweli, inua mkono wako. Sasa aminini.

²²⁹ Huyo mama mweusi aliyeketi wa pili kutoka kwake, hapo amevaa kofia, mama huyo anaugua ugonjwa wa wasiwasi. Mara niliposema hayo kumhusu yeye, alijua habari zake, nayo ikainua imani yake. Kama hiyo ni kweli inua mkono wako, Mama. Unaamini?

²³⁰ Yule mzungu aliyeketi moja kwa moja nyuma ya yule mtu mweusi pale, ambaye ameinua mikono yake. Anamwombea rafiki yake aliye na kansa, anayekufa, naye mtu huyo hayupo hapa, nawe unamwombea, ulianza kuomba mara nilipotaja hilo. Kama hiyo ni kweli, pungu mkono wako *hivi*. Amini, nawe utapata ulichoomba.

²³¹ Je, mnaweza kung'ang'ania? Roho Mtakatifu amepitia jengo lote, akiwaonyesha ya kwamba Yeye anawapenda. Mnaamini? Je, mnang'ang'ania, mnashikilia? Ni wangapi wanaoamini kwa ajili ya uponyaji wenu sasa, wakati Uwepo Wake upo hapa? Huyo ni Yeye. Mmepenya mkaingia sasa, tunaye Yeye mbele zetu. Inueni mikono yenu.

²³² Mama, wewe unayeketi hapo na magongo yamewekwa hapo chini, unayatumia kwa sababu gani? Tupilia mbali vitu hivyo, ama uviache vikae hapo, na uende zako nyumbani. Yesu Kristo anakuponya.

²³³ Mnaamini? Ninaangalia tu mambo yakitukia kwenu. Je, mnaamini? Wekeaneni mikono ninyi kwa ninyi, wekeaneni tu mikono sasa, kila mmoja wenu. Sasa, mtakapokuwa tayari kuondoka, tokeni mle, ondokeni vitini mwenu, kila kitu kingine, aminini tu.

²³⁴ Hivi hamwezi kuvunja kizuizi hicho cha kutokuamini? Tu—tunaweza kuwa wazito namna gani, enyi marafiki? Hivi hamwezi kuona ya kwamba Yesu Kristo, yupo papa hapa sasa, ametufanyia mengi zaidi katika mkutano huu kuliko aliyoandika katika Biblia ambayo aliwahi kufanya? Mnaamini?

Bwana, naamini, Ee Bwana, naamini,
Mambo yote yanawezekana, Ee Bwana,
naamini; (Loo, jambo fulani lilitukia.)
Ee Bwana, naamini, Ee Bwana, naamini,
Mambo yote yanawezekana, Ee Bwana,
naamini.

²³⁵ Kama yuko hapa ama hayuko, sijui, kuna mwanamke anayeomba, ni mke wa mchungaji, ana ugonjwa wa figo, jina lake ni Bibi Miguel. Amini kwa moyo wako wote na unaweza kwenda nyumbani, oponywe.

Bwana, naamini,
Usijali kuhusu hali hiyo ya kanisa, itaondoka pia.
Bwana, naamini, (Loo, enyi watu!)
Mambo yote yanawezekana,
Mnaamini sasa? Je, mnang'ang'ania? Simameni.

. . . naamini;
Ee Bwana, naamini, Ee Bwana, naamini,
Mambo yote yanawezekana, Ee Bwana,
naamini.
Nampenda, na- . . .

²³⁶ Ni wangapi mnaodai uponyaji wenu sasa? Inueni mikono yenu, mkisema, “Kitu hicho kitaniacha. Ninayo imani sasa hivi. Kimeniacha, ninaliamini.”

. . . alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

²³⁷ Kweli, kutoka kwenye kilindi cha moyo wako, unaamini tu kama maskini mwanamke yule Myunani alivyoamini? “Bwana, niko katika Uwepo Wako, ninapokea Neno Lako la ahadi moyoni mwangu, na kama vile tu mwanamke huyo alivyoamini ya kwamba binti yake angekuwa mzima, ninaamini ya kwamba mimi ni mzima na kila haja ambayo nimeomba, ni yangu sasa.” Unaamini hilo? Inua mkono wako, useme, “Mungu, ninakupa mkono wangu wa ahadi, ninaamini kwa moyo wangu wote. Na tangu saa hii na kuendelea, nitang'ang'ania niwezavyo, nimeponywa. Kwa mapigo Yake na ahadi Yake, imani yangu inashikilia Neno la Mungu nami nimeponywa.” Unaamini hilo?

Imani yangu inakutegemea Wewe,
Ewe Mwana-Kondoo wa Kalvari,
Ee Mwokozi, wa Kiungu;

Sasa nisikie ninapoomba,
Ondolea mbali dhambi zangu zote,
Ee nijalie tangu leo
Kuwa Wako kabisa!

²³⁸ Na tuinamishe vichwa vyetu. Kutoka kwenye kilindi cha moyo wako, kutoka kwenye utu wa ndani kabisa ambao unajua chochote kuuhusu, nafsi yenyewe inayokutawala, wewe uliyeinua mkono wako muda mfupi uliopita, wakati nilipotoa wito huo wa madhabahuni, nawe ulitaka Kristo aingie ndani yako, kukufanya Mkristo anayeng'ang'ania, *anayejua hivyo*, sasa unaamini kwamba umepata ulichoomba? Kama unaamini, mwinulie Mungu mkono wako. Kote jengoni, angalieni hiyo mikono, jamani!

²³⁹ Kila mtu aliyekuwa mgonjwa, na bila kusitasita, kama yule Mkushi, ama, si yule mwanamke Mkushi, bali yule mwanamke Msirofoinike, ambaye aliamini kwa moyo wake wote ya kwamba angemkuta binti yake amepona, naye akapona, amini ya kwamba huo ugonjwa, ama shida, chochote ulichokuwa nacho, kwamba Mbele za Kristo alasiri ya leo kwa kuwa Yeye ametubariki kwa kuingia hapa pamoja nasi, amini ya kwamba una imani katika Neno Lake lililoahidiwa la kuwa pamoja nasi, na "ombeni mtakalo mtapewa," nawe umeomba, nawe unaona ishara Yake, kweli unaamini ya kwamba si kanuni fulani ya imani, udanganyifu fulani, wa kimadhehebu, mtabiri fulani, ama mpiga ramli fulani, bali unaamini ni Mwokozi wako, Yesu Kristo, akitenda kazi ndani yako na kukupa imani ya kuliadini, inua mkono wako, useme, "Ninalikubali, na ninaliamini kwa moyo wangu wote."

Kibarikiwe kifungo kiifungayo
Mioyo yetu katika upendo wa Kikristo;
Ushirika wa watu wenye nia moja
Ni kama wa huko Juu.

Mbele ya kiti cha enzi cha Baba yetu,
Tunamwaga maombi yetu kwa bidii;
Hofu zetu, matumaini yetu, malengo yetu ni
mamoja,
Faraja zetu na mahangaiko yetu.

Tunapochana,
Inatupa maumivu ya ndani;
Lakini bado tutaungana moyoni,
Na kutumainia kukutana tena.

²⁴⁰ Mpaka nitakapowaona, Mungu awafanye kung'ang'ania, lichukue Neno Lake kama Mwenge, na Upanga mkononi mwako, na uache imani ilitumie huko nje, na kukata kila giza kutoka kwako, mpaka utakapomwona Yesu katika utimilifu wa baraka Zake. Mungu awabariki.

...kukutana! hata tutakapokutana!

Hata tutakapokutana miguuni pa Yesu; (hata
tutakapokutana!)

Hata tutakapokutana! hata tutakapokutana!
Mungu awe pamoja nanyi hata
tutakapokutana tena! 🕊

62-0520 Kung'ang'ania
Stephen Mather High School
Chicago, Illinois Marekani

SWAHILI

©2024 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org